ACT WAZALENDO

# KATIBA

TOLEO LA 2020

# KATIBA YA ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY (ACT-WAZALENDO)

# KATIBA YA ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY (ACT WAZALENDO) ya 2015 (Toleo la 2020)

# ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY (ACT WAZALENDO)

# KATIBA (TOLEO LA 2020)

Toleo hili ni la kwanza kutolewa tokea katiba hii ya Alliance for Change and Transparency (ACT WAZALENDO) Chama cha Wazalendo kutungwa mwaka 2015.

Toleo hili linajumuisha marekebisho yote yaliyofanywa na kukubaliwa na Mkutano Mkuu uliofanywa Dar es Saalam kuanzia tarehe 14 na 15 Machi, 2020. Pia Marekebisho hayo yanatilia maanani maendeleo ya kisiasa ya Chama chetu na ya Tanzania kwa ujumla ili kukiimarisha zaidi.

Vilevile marekebisho haya yamefanywa kukidhi matakwa ya mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya namba. 5 ya 1992 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 1 ya 2019

Dar es Saalam
17 Machi, 2020

**(Omar Said Shaaban)**
**Mwanasheria Mkuu wa Chama**

# KATIBA YA ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY YA MWAKA 2015

## YALIYOMO

*Ibara* *Kichwa cha Habari*


UTANGULIZI

**SURA YA KWANZA**

JINA, MAKAO MAKUU, ALAMA, ITIKADI, IMANI, MADHUMUNI, LUGHA, MISINGI NA MALENGO YA CHAMA

SEHEMU YA KWANZA

1. Jina la Chama
2. Makao Makuu ya Chama
3. Alama za Chama
4. Itikadi na Falsafa ya Chama
5. Lugha Rasmi ya Chama

SEHEMU YA PILI

6. Misingi ya Chama
7. Malengo na Madhumuni ya Chama

**SURA YA PILI**

UANACHAMA, HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

SEHEMU YA KWANZA

8. Uanachama
9. Mwanachama wa ACT Wazalendo
10. Ada ya Mwanachama
11. Haki za Mwanachama
12. Wajibu wa Mwanachama
13. Kukoma Uanachama
14. Rejesta ya Wanachama
15. Ahadi tano za Mwanachama

**SURA YA TATU**

MUUNDO WA CHAMA, NGAZI ZA CHAMA, NA VIKAO VYA CHAMA

SEHEMU YA KWANZA

MUUNDO NGAZI NA VIKAO VYA CHAMA

16. Muundo wa Chama

SEHEMU YA PILI

NGAZI YA ACT TAWI

17. ACT Tawi
18. Viongozi Wakuu wa ACT Tawi
19. Mkutano Mkuu wa ACT Tawi
20. Kazi na wajibu wa Mkutano Mkuu wa ACT Tawi
21. Kamati ya Uongozi ya ACT Tawi
22. Kazi za Kamati ya Uongozi ya ACT Tawi
23. Vikao vya Kamati ya Uongozi ya ACT Tawi
24. Sekretarieti ya ACT Tawi
25. Kazi za Sekretarieti ya ACT Tawi
26. Kazi za Mwenyekiti wa ACT Tawi
27. Kazi za Katibu wa ACT Tawi
28. Kazi za Mweka Hazina wa ACT Tawi

SEHEMU YA TATU

NGAZI YA ACT KATA/WADI

29. ACT Kata/Wadi
30. Viongozi Wakuu wa ACT Kata
31. Mkutano Mkuu wa ACT Kata
32. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT Kata
33. Kazi na Wajibu wa Mkutano Mkuu wa ACT Kata
34. Kamati ya Uongozi ya ACT Kata
35. Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya ACT Kata
36. Kazi za Kamati ya Uongozi ya ACT Kata
37. Sekretarieti ya ACT Kata
38. Kazi za Sekretarieti ya ACT Kata

39. Kazi za Mwenyekiti wa ACT Kata
40. Kazi za Katibu wa ACT Kata
41. Kazi za Mweka Hazina wa ACT Kata

SEHEMU YA NNE

NGAZI YA ACT JIMBO

42. ACT Jimbo
43. Viongozi wa ACT Jimbo
44. Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo
45. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo
46. Kazi za Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo
47. Kamati ya Uongozi ya ACT Jimbo
48. Kazi za Kamati ya Uongozi wa ACT Jimbo
49. Sekretarieti ya ACT Jimbo
50. Viongozi wakuu wa ACT Jimbo
51. Kazi za Mwenyekiti ACT Jimbo
52. Kazi za Katibu wa ACT Jimbo
53. Kazi za Mweka Hazina wa ACT Jimbo

SEHEMU YA TANO

NGAZI YA ACT MKOA

54. Muundo wa Chama ACT Mkoa
55. Mkutano Mkuu wa ACT Mkoa
56. Kazi za Mkutano Mkuu wa ACT Mkoa
57. Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa
58. Kazi za Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa
59. Sekretarieti ya ACT Mkoa
60. Kazi ya Sekretarieti ya ACT Mkoa
61. Viongozi wa Chama ACT Mkoa

SEHEMU YA SITA

WARATIBU WA CHAMA

62 Waratibu wa Chama
63 Liwali wa Chama wa eneo

64 Kazi za Liwali wa Chama wa eneo
65 Mratibu wa Kanda
66 Kazi za Mratibu wa Kanda

SEHEMU YA SABA

NGAZI YA ACT TAIFA

67 ACT Taifa
68 Vikao vya ACT Taifa
69 Mkutano Mkuu wa ACT Taifa
70 Halmashauri Kuu kuongeza muda wa kufanya Mkutano Mkuu Taifa
71 Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa
72 Kazi za Mkutano Mkuu Taifa
73 Mkutano Mkuu wa Taifa wa Kidemokrasia
74 Halmashauri Kuu ya ACT Taifa
75 Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya ACT Taifa
76 Kazi na wajibu wa Halmashauri Kuu ya ACT Taifa
77 Halmashauri Kuu kuwasimamisha uongozi na wanachama viongozi wakuu
78 Kamati Kuu ya ACT Taifa
79 Kazi za Kamati Kuu ya ACT Taifa
79A. Kamati ya Uongozi ya ACT Taifa na Kazi zake
80 Sekretarieti ya Kamati Kuu Taifa
81 Kamati za Mashauriano

SEHEMU YA NNE

VIONGOZI WA KITAIFA

82 Viongozi wa Kitaifa
83 Kiongozi wa Chama
84 Mwenyekiti wa Chama Taifa
85 Mshauri Mkuu wa Chama
86 Makamu Mwenyekiti na kazi zake
87 Katibu Mkuu
88 Manaibu Katibu Mkuu
89 Mwanasheria Mkuu wa Chama

**SURA YA NNE**

KAMATI MAALUM ZA KAMATI KUU, KAMATI YA MAADILI TAIFA, TAASISI, IDARA ZA CHAMA, NGOME, MAKOSA, NIDHAMU NA UTATUZI WA MIGOGORO.

SEHEMU YA KWANZA

KAMATI MAALUM ZA KAMATI KUU

90 Kamati Maalum za Kamati Kuu
91 Kazi na Wajibu wa Kamati Maalum za Kamati Kuu
92 Wajumbe wa Kamati Maalum za Kamati Kuu

SEHEMU YA PILI

IDARA NA NGOME ZA CHAMA

93 Halmashauri Kuu kuanzisha Idara
94 Ngome za Chama

SEHEMU YA TATU

BODI YA WADHAMINI, KAMATI NA TAASISI NYINGINE

95 Bodi ya wadhamini
96 Kamati na Taasisi nyingine

SEHEMU YA NNE

KAMATI YA MAADILI

97 Kamati za Maadili za Chama
98 Rufaa
99 Kamati ya Maadili ya Taifa
100 Majukumu ya Kamati ya Maadili ya Taifa na Mazingatio ya haki za asili

SEHEMU YA TANO

NIDHAMU MAKOSA NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA CHAMA

101 Maamuzi ya Chama
102 Mapendekezo kutoka ngazi moja ya Chama
103 Utatuzi wa Migogoro

SEHEMU YA SITA

KUSITA KWA MWANACHAMA, KUJIUZULU UONGOZI NA KUFUKUZWA UANACHAMA


104 Kuacha au kuachishwa Uanachama

105 Kujiuzulu Uanachama

106 Kufukuzwa Uanachama


SEHEMU YA SABA

JUMUIYA ZA WABUNGE, WAWAKILISHI NA MADIWANI


107 Jumuiya za Wabunge, Wawakilishi na Madiwani

108 Kiongozi wa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani


**SURA YA TANO**

UCHAGUZI NA TARATIBU ZAKE KATIKA CHAMA, ELIMU KWA WANACHAMA


109 Uchaguzi wa Viongozi wa Chama

110 Wajibu wa Chama kuelimisha

111 Masharti ya kuchaguliwa na kipindi cha Uongozi


**SURA YA SITA**

FEDHA ZA CHAMA, MAPATO NA MALI ZA CHAMA


112 Fedha, Mapato na Mali za Chama

113 Malipo na utaratibu wake


**SURA YA SABA**

MENGINEYO

SEHEMU YA KWANZA

MAREKEBISHO YA KATIBA NA KANUNI


114 Marekebisho ya Katiba

115 Kanuni za Chama


SEHEMU YA PILI

KUKAIMU MADARAKA, KUKASIMU MADARAKA, KUVUNJWA KWA CHAMA NA MAMBO MENGINEYO


116 Kukaimu madaraka

117 Kuvunjwa kwa Chama

118 Ofisi zilizoanzishwa
119 Akidi na uhalali wa vikao
120 Mialiko kwa wadau, wataalamu na watu wengine
121 Uwezo wa kuunda Kamati
122 Wajibu wa Kiongozi wa Serikali kwa tiketi ya Chama
123 Mahudhurio ya kikao cha Chama
124 Kujaza nafasi zilizowazi
125 Ofisi za Viongozi wa Chama
126 Upeperushaji wa bendera ya Chama
127 Kukasimu madaraka
128 Uteuzi na masuala ya kijinsia na makundi maalum

SEHEMU YA TATU

TAFSIRI YA MANENO MBALIMBALI NA UFAFANUZI KWA BAADHI YA MAENEO

129 Ufafanuzi na Tafsiri ya maneno mbalimbali

SEHEMU YA NNE

JINA LA KATIBA, TAREHE YA KUTUMIKA NA UHALALISHAJI WA MAMBO YALIYOKWISHA KUFANYIKA CHINI YA KATIBA HII KABLA YA KUFANYIWA MAREKEBISHO

130 Jina la Katiba na kuanza kutumika
131 Utekelezaji wa vifungu mbali mbali
132 Kuhalalisha mambo fulani
133 Uhalalishaji wa kanuni
134 Usawazishaji wa makosa ya uandishi au uhamisho wa Ibara kabla ya kuchapwa kwa Katiba

## SURA YA KWANZA

## JINA, MAKAO MAKUU, ALAMA, ITIKADI, IMANI, MADHUMUNI, LUGHA, MISINGI NA MALENGO YA CHAMA

### SEHEMU YA KWANZA

### JINA, MAKAO MAKUU, ALAMA, ITIKADI, IMANI, MADHUMUNI NA LUGHA

*Jina la Chama*

1. (1) Jina la Chama litakuwa ni ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY ambalo kwa ufupisho litatamkwa kama ACT Wazalendo.

(2) Kwa mujibu wa katiba hii, maneno ACT na ACT Wazalendo yanapotajwa, basi ieleweke kuwa ni Chama cha Alliance for Change and Transparency.

*Makao Makuu ya Chama*

2. (1) Makao Makuu ya Chama yatakuwa ni Dar es Salaam.

(2) Kutakuwa na ofisi kuu ya Makao Makuu Zanzibar.

(3) Kutakuwa na ofisi ndogo za Makao Makuu ambazo zitakuwa na waratibu wa Chama katika Mikoa ya Mwanza, Dodoma na Pemba.

(4) Bila ya kuathiri Masharti ya Katiba hii Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza pindi ikiona inafaa kuanzisha ofisi nyingine ndogo ya Makao Makuu katika eneo lolote lile ambalo itaona inafaa.

(5) Anuani za ofisi zote hizo, pamoja na Makao Makuu ya Chama zitakuwa kama zitakavyoamuliwa na Kamati Kuu.

(6) Kanda ni eneo lililotamkwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kuwa ni sehemu ambayo inasimamiwa kichama na Mratibu, na inaweza kuwa ni eneo la mkoa mmoja au zaidi

*Alama za Chama*

3. (1) Alama za Chama zitakuwa ni:
   i) Rangi za chama ambazo ni zambarau na nyeupe;
   ii) Bendera ya Chama ambayo itakuwa ni ya rangi ya Zambarau na nyeupe ikiwa na nembo ya chama katikati ya bendera
   iii) Nembo ya Chama
   iv) Wimbo rasmi wa chama
   v) Vazi rasmi la chama.

(2) Halmashauri Kuu ya Chama itatengeneza kanuni kufafanua muundo na yaliyomo ndani ya nembo ya chama, wimbo rasmi wa Chama na vazi rasmi la chama.

(3) Halmashauri Kuu itakuwa na uwezo wa kubadili alama za chama kutokana na mahitaji ya wakati

*Itikadi na Falsafa ya Chama*

4. (1) ACT Wazalendo inaamini katika itikadi ya Ujamaa wa Kidemokrasia (Democratic Socialism) ikiwa na ngao nne zifuatazo:

(i) Udugu ni hifadhi ya jamii ya asili kwa Afrika, na hivyo kila mtanzania na kila mwafrika ana jukumu la kumsaidia mwenzake anayekabiliwa na tatizo au janga popote alipo bila kutarajia malipo ya aina yoyote;

(ii) Serikali ina haki na wajibu wa kutengeneza sheria na kanuni zenye kulenga na kuleta usawa wa kibinadamu na fursa za maendeleo katika jamii. Aidha, Serikali ina haki na wajibu wa kusimamia moja kwa moja sekta nyeti katika jamii zenye maslahi mapana ya kiusalama na kiuchumi kwa nchi. Pamoja na kutambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika uchumi na maisha ya kijamii kwa ujumla, ACT Wazalendo inaamini kwamba serikali inawajibika kupitia mfumo wa kisheria kuhakikisha kwamba kila mwananchi anakuwa na fursa sawa za kujiletea maendeleo na kupata huduma muhimu

za kijamii na kwamba serikali ina wajibu wa msingi wa kuwakinga wananchi kupitia mfumo wa sheria dhidi ya athari zitokanazo na soko huria;

(iii) Viongozi na watumishi wa umma wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wanaishi na kuenenda katika misingi inayolinda heshima ya ofisi za umma na kwamba hawatumii nafasi zao kwa manufaa yao binafsi na jamaa zao. Ili kuwasaidia na kuwawezesha viongozi na watumishi wa umma kuenenda katika misingi ya maadili, kuna haja ya kuwekewa miiko na maadili maalumu ya viongozi; na

(iv) Demokrasia ndiyo msingi wa maendeleo, umoja na maelewano katika jamii ya watu waliostaarabika. Katika hili, ACT Wazalendo inaamini kwamba msingi mama wa demokrasia ni kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa huru na kwamba sauti zao zinasikika na kuzingatiwa katika mipango ya maendeleo ya nchi. Aidha, ACT Wazalendo inaamini katika kudumisha utawala wa sheria.

(2) Falsafa ya ACT Wazalendo ni **Siasa ni Maendeleo** ikiwa na dhamira ya kurudisha, kuhuisha na kupigania misingi ya utu, usawa na heshima ya binadamu ikiwa ina imani kwamba:

(i) Binadamu wote ni sawa;
(ii) Kila mtu anastahili heshima;
(iii) Kila raia ana uhuru kamili wa kutoa mawazo yake, kwenda anakotaka na kuamini dini anayotaka na kukutana na watu wengine bila kuvunja sheria;
(iv) Kila mtu ana haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria;
(v) Kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake;
(vi) Raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao na

vizazi vijavyo; na

(vii) Serikali ina mamlaka na wajibu wa kusimamia njia muhimu za kukuza uchumi.

*Lugha rasmi ya Chama*

5. (1) Lugha rasmi ya chama itakuwa ni Kiswahili.

(2) Bila kuathiri ibara ndogo ya (1) ya ibara hii, lugha ya Kiingereza inaweza kutumika sambamba na lugha ya Kiswahili inapobidi.

(3) Nyaraka zote muhimu, ikiwemo Katiba hii, zitaandikwa katika lugha ya Kiswahili na pale inapohitajika zinaweza kutafsiriwa katika lugha ya Kiingereza au lugha nyingineyo ikiwa kwa kufanya hivyo kutasaidia mawasiliano na maelewano zaidi katika kufanikisha shughuli za Chama.

(4) Chama kinaweza kuweka mazingira yatakayowezesha kuwepo kwa mawasiliano mbadala zikiwemo lugha za alama kwa kadri ya mahitaji.

## SEHEMU YA PILI

## MISINGI NA MALENGO YA CHAMA

*Misingi ya Chama*

6. (1) ACT itaongozwa na Misingi ifuatayo:-

i. Uzalendo
ii. Usawa
iii. Kupinga na Kupiga Vita ubaguzi
iv. Uadilifu
v. Uwazi
vi. Uwajibikaji
vii. Demokrasia
viii. Uhuru wa Mawazo na Matendo
ix. Utu
x. Umoja

(2) Katiba hii ya ACT ipo kwa ajili ya kuilinda misingi hii muhimu ya Chama na hivyo ibara yoyote ya Katiba hii ni lazima ilenge katika malengo hayo.

(3) Misingi hii itafafanuliwa katika nyaraka mbalimbali zitakazotolewa na Chama kwa mujibu wa Katiba hii, miongozo na Kanuni za uendeshaji wa Chama.

*Malengo na Madhumuni ya Chama*

7. Shabaha kuu ya ACT ni kuhakikisha kuwa utajiri wa nchi unatumika kuimarisha zaidi maisha ya watu na kuchochea uwezo wao katika kuchangia na kujenga uchumi shirikishi ambapo kila mtu ana fursa sawa za maendeleo. Ili kufikia shabaha hii, ACT Wazalendo itapambana kuhakikisha kwamba inashinda uchaguzi na kuunda serikali ili kutekeleza malengo yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kwamba serikali inatumia rasilimali zote za nchi kwa ajili ya kuondosha umaskini, ujinga, maradhi, rushwa, na kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla;

(ii) Kupigania na kulinda uongozi bora na Utawala wa Sheria;

(iii) Kujenga, kukuza na kuendeleza demokrasia, raslimali za nchi na serikali inayowajibika kwa umma wa Watanzania;

(iv) Kuhakikisha usawa kwa raia wote, wanaume kwa wanawake bila kujali kabila, rangi, imani za kidini, itikadi, utamaduni ama hadhi ya mtu kiuchumi na kijamii;

(v) Kuendeleza na kudumisha demokrasia na utamaduni wa mfumo wa vyama vingi vya siasa;

(vi) Kuchochea, kuimarisha na kulinda uzalendo, maadili, uwajibikaji na uwazi kama misingi mikuu katika uongozi wa nchi;

(vii) Kuchochea na kuendeleza mapambano katika kulinda haki za watoto, wanawake na watu wenye ulemavu;

(viii) Kupigania haki na heshima ya wafanyakazi, wakulima, wafugaji na wajasiriamali katika ngazi zote;

(ix) Kudhibiti soko huria ili kuhakikisha kuwa haliathiri haki za utu za wafanyakazi na watu wenye kipato cha chini;

(x) Kulinda na kuendeleza mazingira bora kwa vizazi vya leo na vijavyo;

(xi) Kuhakikisha kuwa idhini, mikataba na ushirikiano wa kikanda barani Afrika ambavyo Tanzania ni mwanachama kama vile Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) vinaendana na misingi mikuu ya kidemokrasia na kuendeleza na kuheshimu usawa na utu wa Afrika;

(xii) Kuhimiza ushirikiano na mahusiano na vyama vingine vinavyoamini katika ujamaa wa kidemokrasia katika Afrika na duniani kote;

(xiii) Kuunga mkono na kusukuma mbele juhudi za kuundwa kwa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki na kupigania umoja wa Afrika.

(xiv) Kuulinda, kuutetea na kuimarisha muungano wa nchi zetu mbili za Tanganyika na Zanzibar katika njia za haki na usawa kwa kila upande, na

(xv) Kulinda, kutetea na kudumisha Mapinduzi ya Zanzibar katika kulitimiza lengo la Mapinduzi hayo na kuhakikisha kwamba Zanzibar kama nchi iliyoungana na Tanganyika inadumu na malengo yake ya kuwatetea wanyonge na kuleta usawa kwa wananchi wote.

## SURA YA PILI

## UANACHAMA HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA
## SEHEMU YA KWANZA

*Uanachama*

8. (1) Uanachama wa ACT utakuwa wazi kwa mtu mwenye sifa zifuatazo:

(a) Awe ni raia wa Tanzania;
(b) Awe ana akili timamu na amefikia umri wa miaka 18 au zaidi;
(c) Awe anakubaliana na falsafa, itikadi, misingi, madhumuni na sera za ACT;
(d) Awe na moyo na utayari wa kukitumikia Chama na uzalendo kwa nchi yake;
(e) Asiwe mwanachama wa chama kingine cha siasa baada ya kujiunga na ACT;

(2) Mtu yeyote anayeomba kuwa mwanachama wa ACT Wazalendo:
(a) Atajaza fomu ya maombi na kuiwasilisha kwenye Tawi lililopo katika eneo lake.
(b) Ataorodheshwa katika rejista la wanachama la Tawi hilo pindi ikiwa amekubaliwa.
(c) Mara baada ya kukubaliwa ombi lake atalipa kiingilio na kupewa kadi ya uanachama na kulipa ada kama zitakavyoamuliwa na Halmashauri Kuu ya Chama.

(3) Mtu aliyekataliwa kuwa mwanachama anaweza kuomba tena baada ya kipindi cha miezi sita kupita na akikataliwa mara ya pili, anaweza kukata rufaa kwenye ngazi ya Kata au Jimbo ambalo Tawi lake limo, kama atakataliwa anaweza kukata rufaa kwenye ngazi ya Mkoa kwa uamuzi wa mwisho.

(4) Mamlaka yote ya kuingiza mwanachama mpya katika Chama yatakuwa chini ya Tawi ambalo mwanachama huyo anaishi au ameomba kuwa mwanachama wa Tawi hilo.

(5) Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (4) hapo juu, kiongozi yeyote wa Chama au Serikali anayetokana na Chama anaweza kumpokea mtu au watu kuwa wanachama wapya pindi atakapokuwa katika mkutano wa hadhara au ziara za ujenzi wa Chama.

(6) Mwanachama au wanachama waliopata uanachama chini ya masharti ya ibara ndogo ya (5) hapo juu, watatakiwa kukamilisha matakwa yote ya Katiba kama yalivyoainishwa

katika kifungu cha 8(2) (a), (b) na (c) cha Katiba hii ndani ya siku kumi na nne tangu siku walipopokelewa.

*Mwanachama wa ACT Wazalendo*

9. Mwanachama wa ACT Wazalendo ni mtu yeyote aliyejiandikisha kuwa mwanachama na akakubalika, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuwa mwanachama halali wa chama hiki.

*Ada ya Uanachama*

10. (1) Kila mwanachama atawajibika kulipa ada ya uanachama kama itakavyoainishwa kwenye Kanuni za Uendeshaji wa Chama zitakazotungwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama.

(2) Bila kuathiri Sheria zinazohusu vyama vya siasa nchini, pamoja na misingi na masharti ya Katiba hii, kila mtu au kundi la watu wanaokubaliana na itikadi, misingi, madhumuni na sera za ACT wanaweza kutoa ada ya kundi la uanachama.

(3) Kutakuwa na kiingilio kwa kila mwanachama na kundi lolote litakalotaka kujiunga na Chama kama itakavyoainishwa kwenye Kanuni za Uendeshaji wa Chama.

(4) Utaratibu wa ulipaji wa kiingilio na ada utafafanuliwa katika Kanuni za Uendeshaji wa Chama.

*Haki za Mwanachama*

11. Kila mwanachama wa ACT Wazalendo atakuwa na haki zifuatazo:-

(1) Kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote za Chama zinazomhusu.

(2) Kuhudhuria, kushiriki katika mijadala ya vikao vya Chama na kupiga kura pale anapohusika katika vikao vinavyomhusu ambavyo ni mjumbe.

(3) Kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi, ujumbe au uwakilishi wa Chama, au Serikali kwa kupitia Chama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Kanuni zilizowekwa.

(4) Kuonana na kiongozi yeyote wa Chama kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

(5) Kujitetea mbele ya chombo chochote cha Chama

kinachotaka kumchukulia hatua za kinidhamu, na kuomba kukata rufaa hadi kufikia ngazi ya mwisho ikiwa hataridhishwa na uamuzi uliokwishatolewa.

(6) Kumkosoa kiongozi, mwanachama au mfanyakazi wa Chama kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

(7) Kuwasilisha pendekezo au maelezo kwenye kikao chochote cha Chama, hadi katika ngazi ya Halmashauri Kuu;

(8) Kusikilizwa na kuuliza maswali kuhusu maendeleo na mwenendo wa Chama;

*Wajibu wa Mwanachama*

12. Kila mwanachama wa ACT atakuwa na wajibu ufuatao:-

(1) Kuisoma, kuifahamu, kuitetea na kuiheshimu Katiba hii na kuyatekeleza masharti yake yote, ikiwa ni pamoja na Kanuni zitakazotungwa.

(2) Kuijua, kuikubali, kuilinda na kuitetea Falsafa na Itikadi ya Chama.

(3) Kuyafahamu malengo ya Chama na kuyaunga mkono na kuyatetea.

(4) Kukieneza Chama kwa kuwashawishi wananchi kujiunga na Chama kwa kuzieneza sera za Chama kwa uwezo wake wote.

(5) Kukiunga mkono Chama kwa kuwapigia kura wanachama waliowekwa na Chama kwa ajili ya kugombea nafasi yoyote katika uchaguzi wa nchi utakaohusisha vyama vingine vya siasa.

(6) Kulinda heshima ya Chama kwa kuwa na tabia njema, kutekeleza masharti ya Katiba ya Chama, kutii Kanuni za Chama, kutii Sheria na Sheria ndogo ndogo za Serikali iliyoundwa kihalali na pia, kwa busara, kukosoa utekelezaji mbaya wa Serikali kwa hoja za msingi ili kuendeleza maslahi ya Chama, maslahi yake mwenyewe, maslahi ya wanachama wenzake, maslahi ya nchi na maslahi ya raia wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(7) Kuwa mwaminifu kwa Chama na Serikali zilizoundwa kihalali na kwa ridhaa ya wananchi na kuwa tayari kuwatumikia watu kwa juhudi, maarifa, na vipaji vyake

vyote.

(8) Kuhudhuria vikao vya Chama vinavyomhusu na vile alivyoalikwa kwa barua, simu, nukushi, barua pepe, ujumbe wa Afisa wa Chama au njia nyingine inayokubalika kama itakavyoelezwa na Kanuni za Chama.

(9) Kuimarisha umoja na kujenga mapenzi baina ya wananchi.

(10) Kuwa tayari kupambana na namna yoyote ya uonevu, ukandamizaji, udhalilishaji na ubaguzi.

(11) Kujielimisha zaidi ili aweze kumudu dhamana zote atakazopewa na Chama au dola ili azitekeleze vyema kwa maslahi ya wanachama na wananchi wote wa Tanzania.

(12) Kulinda, kupigania haki za kijamii na kutetea haki za binadamu nchini kwa mtu yeyote au mahali popote duniani pale anapoonewa, kudhalilishwa au kudhulumiwa.

(13) Kutumia uhuru na haki zake bila kuingilia uhuru na haki za wenzake na kuheshimu maoni ya wengine.

(14) Kushirikiana na serikali halali ya nchi na kujitolea muhanga nafasi yake pale adui wa nje anapoivamia au kuihujumu nchi yetu kwa uhasama, ubabe na matumizi ya nguvu yanayoweza kuleta madhara kwa wananchi na nchi.

(15) Kushiriki kikamilifu katika kuzuia na kukilinda Chama kutokana na maadui wa ndani au wa nje wanaokusudia kukihujumu, kukigawa, kukidhoofisha au kuhatarisha uhai wa Chama.

(16) Kuwa mfano na sura ya ACT kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi na umakini.

(17) Kulipa ada na kuchangia mchango wowote kwa kazi maalum zilizokubaliwa na Halmashauri Kuu au na ngazi nyingine za Chama kama itakavyokuwa imeamuliwa na vikao vya Chama.

*Kukoma Uanachama*

13. (1) Mwanachama atakoma kuwa mwanachama ikiwa:

(i) Atajiuzulu mwenyewe kwa hiari yake kwa kuandika

barua kwa Katibu wa ngazi yake au Katibu Mkuu kwa kueleza uamuzi wake wa kuacha kuwa mwanachama.

(ii) Atajiunga na chama kingine cha siasa;

(iii) Atafukuzwa uanachama kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zilizowekwa.

(iv) Atapoteza sifa za uanachama kama zilivyoainishwa katika Katiba hii.

(v) Amefariki.

(2) Mwanachama anaweza kusimamishwa uanachama ili kupisha uchunguzi utakaofanywa na Kamati ya Maadili katika ngazi husika kuhusu mwenendo wake.

(3) Mwanachama anaweza kufukuzwa kwenye Chama kwa sababu zinazotokana na mwenendo usiofaa kwa mujibu wa masharti na Kanuni za Katiba hii, na mara baada ya kufukuzwa, uanachama wake utakoma.

(4) Pamoja na sababu nyingine kama zilivyoelezwa katika Katiba hii na Kanuni zitakazotungwa na Halmashauri Kuu, mwanachama yeyote ambaye atasaidia, kushawishi, kujiunga, kutoa tamko la kuunga mkono chama kingine au mgombea wa chama kingine wakati Chama kimeweka mgombea kwenye uchaguzi wowote kwa mujibu wa Sheria ya nchi atakuwa amepoteza uanachama wa ACT.

(5) Hakuna mwanachama atakayesimamishwa au kufukuzwa uanachama hadi pale ambapo masharti yaliyoainishwa katika Katiba hii na Kanuni za Uendeshaji wa Chama yatakapokuwa yamefuatwa.

(6) Uamuzi wa kumsimamisha uanachama ama kumfukuza mwanachama yeyote hautakuwa na nguvu hadi pale uamuzi huo utakapokuwa umewasilishwa kwa mwanachama husika kwa maandishi.

(7) Bila kuathiri ibara ndogo ya (6) ya ibara hii, mwanachama ambaye atakataa kupokea taarifa ya maandishi juu ya

uamuzi wa kusimamishwa au kufukuzwa uanacahama uliochukuliwa dhidi yake, atahesabika kwamba ameshawasilishiwa taarifa hiyo kwa mujibu wa ibara ndogo ya (6) na uamuzi wa kumsimamisha au kumfukuza uanachama utakuwa na nguvu.

(8) Kila mtu ambaye amekoma kuwa mwanachama atalazimika kurudisha mali za Chama zilizo chini yake ikiwa ni pamoja na kadi ya uanachama.

(9) Mwanachama aliyefukuzwa uanachama kwa mujibu wa Katiba hii hatarudishiwa ada, michango na mali nyingine ambazo atakuwa amechangia alipokuwa mwanachama.

(10) Pale mwanachama atakapokuwa amepoteza uanachama wake kwa mujibu wa Katiba hii anaweza kuomba tena uanachama baada ya miezi sita.

(11) Mwanachama aliyejiuzulu kama ilivyoainishwa katika ibara ya 13(1) hapo juu, atahesabika kuwa amekoma kuwa mwanachama kuanzia tarehe ya barua yake ya kujiuzulu.

*Rejesta ya Wanachama*

14. (1) Kutakuwa na rejesta ya wanachama wote katika kila Tawi, Kata/Wadi na kila Jimbo la Uchaguzi, na rejesta hii itahuishwa kila baada ya miezi sita na Katibu wa Chama katika ngazi husika atatuma orodha ya wanachama kwa ngazi inayofuata kwa ajili ya kumbukumbu za Chama katika kila ngazi.

(2) Katibu wa Chama Mkoa atatunza rejesta ya wanachama wote kwenye mkoa wake na atapokea orodha ya wanachama wote walioandikishwa kila jimbo katika mkoa wake.

(3) Sekretarieti ya Chama Makao Makuu itatunza rejesta ya wanachama wote kwa nchi nzima.

*Ahadi tano za Mwanachama*

15. Kila mwanachama wa ACT atatoa ahadi tano zifuatazo kwa utaratibu ambao utawekwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa.

(i) Nitapambana dhidi ya dhulma, fitina, unafiki uongo, rushwa na ufisadi kwa uwezo wangu wote;

(ii) Nitapambana dhidi ya umasikini na nitasimamia utajiri wa nchi yangu kwa faida ya wote;

(iii) Nitashiriki kujenga Taifa lenye kujitegemea, lisilo na unyonyaji, ubaguzi na lenye misingi ya Haki;

(iv) Nitashiriki kujenga Umoja wa Afrika; na

(v) Nitapigania kuwepo kwa Demokrasia ndani na nje ya Chama changu.

*Muundo wa Chama*

16. (1) Ili kuwa karibu na wanachama, muundo wa Chama utakuwa na ngazi zifuatazo;-

(a) Ngazi ya ACT Tawi
(b) Ngazi ya ACT Kata kwa Tanzania Bara
(c) Ngazi ya ACT Jimbo
(d) Ngazi ya ACT Mkoa
(e) Ngazi ya ACT Taifa

(2) Mbali na Muundo wa Chama ulioainishwa katika Ibara ndogo ya (1) ya ibara ya 16 ya Katiba hii, kutakuwa na Muundo wa Kanda kama itakavyoamuliwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa.

(3) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza, ikiona inafaa kuongeza au kupunguza ngazi yoyote ile kwa eneo lolote lile kwa Tanzania nzima au kwa Tanzania Bara pekee au Zanzibar pekee.

(4) Uundaji wa ngazi moja ya Chama utafanyika baada ya kuwa na muundo na uongozi katika ngazi za chini kwa angalau asilimia 40 kwa mfano kwamba, ili kuunda ngazi ya Kata ni lazima kuwe na angalau asilimia 40 ya matawi yenye uongozi katika Kata husika.

(5) Kwa kuzingatia Ibara ndogo ya (1) hapo juu, ngazi ya juu ya Chama itateua Kamati ya muda itakayokuwa na wajibu wa kuratibu shughuli za Chama na kuwaunganisha wanachama katika eneo lisilo na uongozi wa kikatiba kwenye ngazi ya

chini mpaka wanapofikia uwezo wa kuwa na uongozi kwa mujibu wa Katiba hii.

(6) Ngazi ya Chama ya Taifa itakuwa ni mkaguzi wa ngazi ya Chama zilizoko chini yake, na kwa mpangilio huo huo kila ngazi iliyoko juu itakuwa ni mkaguzi wa Chama kwa ngazi zilizoko chini yake.

## SEHEMU YA PILI

## NGAZI YA TAWI

*ACT Tawi*

17. Tawi linaweza kuanzishwa mahali popote pale ambapo patakuwa na wanachama walio hai wasiopungua hamsini, kwa Zanzibar na ishirini kwa Tanzania Bara ila ijulikane kwamba pale inapokuwa katika Tawi hilo wanachama wake wanazidi mia nne kwa Zanzibar au mia moja kwa Tanzania Bara, basi Kamati ya Uongozi ya Jimbo kwa Zanzibar au Kamati ya Uongozi ya Kata kwa Tanzania Bara inaweza, ikiona inafaa na kwa maslahi ya Chama kuidhinisha kwa maandishi kuanzishwa kwa Tawi jingine katika eneo hilo.

Isipokuwa kwamba, ikiwa uamuzi wa kuanzisha Tawi jipya chini ya Ibara hii utafikiwa chini ya miezi sita kuelekea uchaguzi mkuu, utatakiwa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Chama ndani ya siku 7 (saba) kuanzia tarehe ya Uamuzi kwa ajili ya kuridhiwa.

*Viongozi Wakuu wa ACT Tawi*

18. Kila Tawi litakuwa na viongozi wafuatao:-
  a. Mwenyekiti wa ACT Tawi;
  b. Katibu wa ACT Tawi.

*Mkutano Mkuu ACT Tawi*

19. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Tawi ambao utakutana katika vikao vyake vya kawaida mara moja baada ya kila miezi sita, na kwamba Kamati ya Uongozi ya Tawi inaweza ikiona ni muhimu na pana dharura ya kutosha kwa kuita Mkutano Mkuu, basi Kamati ya Uongozi ya Tawi itaitisha Mkutano Mkuu huo.

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi watakuwa ni viongozi

wote pamoja na wanachama wote wa Chama waliopo katika Tawi hilo.

*Kazi na wajibu wa Mkutano Mkuu wa ACT Tawi*

20. Kazi na Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Tawi zitakuwa kama zifuatavyo:-

a. Kuchagua viongozi wa Tawi waliotajwa katika Ibara ya 18 isipokuwa;

   i. Viongozi wa Ngome zote za Chama ambao watachaguliwa kwa mujibu wa taratibu na Kanuni za Ngome hizo.

   ii. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge, Madiwani pamoja na Wabunge na Wawakilishi na Madiwani wa Viti Maalumu ambao utaratibu wao wa kuchaguliwa umeelezwa katika kanuni za uchaguzi zilizotungwa kwa ajili hiyo.

b. Kupiga kura ya maoni na kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji;

c. Kujadili taarifa ya Kamati ya Uongozi ya Tawi na kutoa maamuzi au maelekezo ya utekelezaji;

d. Kuchagua wajumbe wawili; mmoja akiwa ni mwanamke, watakaoingia katika Mkutano Mkuu wa Kata kwa Tanzania Bara na Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa Zanzibar;

e. Kupokea maamuzi na maagizo ya vikao vya juu vya Chama na kutoa maelekezo kwa Kamati ya Uongozi ya Tawi kwa utekelezaji;

f. Kujadili utekelezaji wa itikadi, falsafa, sera na mipango ya Chama inayohusu masuala ya jamii katika eneo la kijiji, mitaa iliyomo katika Tawi hilo;

g. Kutoa mwongozo na maelekezo kwa wawakilishi wa Chama walio kwenye Serikali ya Kijiji au Kamati ya

Mtaa;

h. Kujadili na kuzingatia taarifa za utendaji wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee katika Tawi na kutoa maelekezo; na

i. Kuidhinisha programu za Chama katika eneo lao.

*Kamati ya Uongozi ya ACT Tawi*

21. (1) Kutakuwa na Kamati ya Uongozi ya ACT Tawi itakayokuwa na viongozi wafuatao:

a. Mwenyekiti;
b. Katibu;
c. Mweka hazina;
d. Katibu wa Mawasiliano na Uenezi;
e. Katibu wa Mipango na Chaguzi;
f. Wenyeviti wa Ngome wa ACT Vijana, Wanawake na Wazee;
g. Makatibu wa Ngome wa ACT Vijana, Wanawake na Wazee;
h. Wajumbe wanne, wawili wanaume na wawili wanawake watakaoingia katika Kamati ya Uongozi ambao watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi;
i. Mwakilishi, Mbunge na Diwani na viongozi wa Serikali za Mitaa, vijiji na vitongoji wanaotokana na Chama cha ACT ambao wanaishi katika Tawi hilo;
j. Liwali wawili wa maeneo katika Tawi ambao watachaguliwa na kamati ya uongozi ya Tawi mmoja wao akiwa ni mwanamke.

(2). Pale ambapo Mwenyekiti wa Kijiji, au Mtaa anayetokana na Chama, au kuwa Mwakilishi wa Wenyeviti au Wajumbe wa Serikali za Mitaa au Vijiji anaishi katika Tawi hilo, basi naye kwa nafasi hiyo atakuwa ni mjumbe wa Kamati ya Uongozi.

*Kazi za kamati ya Uongozi wa ACT Tawi*

22. Kazi za Kamati ya Uongozi ya Tawi zitakuwa ni kama zifuatavyo:-

a. Kuendesha shughuli za kila siku za Chama katika Tawi;

b. Kuandaa Mkutano Mkuu wa Tawi na ajenda zake;

c. Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza itikadi, falsafa, sera na madhumuni ya Chama;

d. Kuendesha na kusimamia Kampeni za Uchaguzi wa wagombea wa Chama katika Uchaguzi wa Kiserikali;

e. Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya Tawi husika;

f. Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama; na

g. Kuhakikisha Chama kinashinda kwenye uchaguzi wowote ule unaohusika na kinapata kura nyingi za Mwenyekiti wa kijiji/kitongoji/mtaa, Ubunge, Uwakilishi na Urais katika ngazi ya Tawi husika.

*Vikao vya kamati ya Uongozi*

23. Kamati ya Uongozi ya Tawi itakutana angalau mara moja kwa kila mwezi, lakini wanaweza kukutana wakati wowote watakaoupanga na kukubaliana wakiona kuna haja ya kufanya hivyo.

*Sekretarieti ya ACT Tawi*

24. (1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Tawi ambayo itakutana kila siku au kwa siku na wakati watao kubaliana.

(2) Wajumbe wa Sekretarieti ya Tawi watakuwa:

a. Katibu wa Tawi ambaye ni Mwenyekiti wa Sekretarieti;

b. Katibu Mwenezi wa Tawi atakuwa ni Katibu wa Sekretarieti;

c. Mweka hazina wa Tawi;

d. Katibu wa Mipango na Chaguzi;

e. Katibu wa Ngome ya Vijana;

f. Katibu wa Ngome ya Wanawake;

g. Katibu wa Ngome ya Wazee;

*Kazi ya Sekretarieti ya ACT Tawi*

25. Kazi ya Sekretarieti ya Tawi zitakuwa kama zifuatazo:

a. Kuandaa Kikao cha Kamati ya Uongozi ya Tawi na agenda zake;
b. Kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Chama katika Tawi;
c. Kuandaa mikakati na kuishauri Kamati ya Uongozi ya Tawi juu ya kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali;
d. Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza itikadi, falsafa, sera na madhumuni ya Chama;
e. Kutekeleza maamuzi ya vikao vya Tawi na ngazi za juu za Chama;
f. Kuweka kumbukumbu sahihi za wanachama katika rejesta ya wanachama kwa mujibu wa Kanuni za Chama;
g. Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama katika Tawi na kuziwasilisha kwenye ngazi za juu kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

*Kazi za Mwenyekiti ACT Tawi*

26. Kazi za Mwenyekiti wa Tawi zitakuwa kama zifuatazo:-

a. Atakuwa Mwenyekiti wa mikutano na vikao vyote vya Tawi;

b. Atakuwa msemaji mkuu wa Chama katika Tawi;

c. Atakuwa ndiye mhamasishaji mkuu wa siasa ya Chama katika eneo lake;

d. Katika mikutano anayoongoza, zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, atakuwa pia na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasiofiki zitalingana; na

e. Atahakikisha kuwa Chama kinashinda ngazi ya Tawi katika uchaguzi wa serikali za mitaa au

Uchaguzi wowote ulioidhinishwa na Chama.

*Kazi za Katibu wa Tawi*

27. Kazi za Katibu wa Tawi zitakuwa kama zifuatazo:-

a. Atakuwa Katibu wa mikutano na vikao vyote vya Tawi;
b. Atawajibika kuandaa na kutoa taarifa ya kila mwezi kuhusu utendaji wa shughuli za Chama katika Tawi;
c. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Tawi;
d. Atakuwa Mdhibiti Mkuu wa mali za Chama katika Tawi;
e. Atatunza, nyaraka za Chama, rejesta ya wanachama wote waliopo katika Tawi lake;
f. Ataitisha vikao vya tawi vya Kamati ya Uongozi na Mkutano Mkuu kwa maelekezo ya Sekretariat na Kamati ya Uongozi;
g. Atakuwa ndiye mwajibikaji mkuu wa masuala yote yanayohusu fedha na mali za Chama katika eneo lake; na
h. Kuhakikisha kuwa Chama kinashinda katika uchaguzi wa kiserikali au uchaguzi mwengine wowote ulioidhinishwa na Chama.

*Kazi za mweka hazina wa ACT Tawi*

28. Kazi za Mweka hazina wa Tawi zitakuwa kama zifuatazo:-

a. Kwa niaba ya Katibu wa Tawi, atatunza mali na fedha za Chama na madaftari ya mahesabu yote ya fedha na ya mali za Chama na kuyaweka tayari kwa ukaguzi wa ndani ya Chama wakati wote;
b. Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumzi ya kila mwaka ya Chama katika Tawi;
c. Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya Tawi na ngazi za juu;
d. Kubuni miradi ya uchumi katika Tawi na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya Chama vya ngazi ya Tawi na ngazi za juu;

e. Kukusanya mapato ya Chama katika Tawi na kufanya malipo yote yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha na taratibu nyengine za Chama kama zilivyowekwa katika Kanuni zitakazotungwa na Kamati Kuu ya Taifa na kuidhinishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

## SEHEMU YA TATU

## NGAZI YA KATA

*ACT Kata*

29. (1). Kutakuwa na ngazi ya Kata ya Chama kwa upande wa Tanzania Bara, pale ambapo kiutawala kwa mujibu wa sheria za serikali za Mitaa za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pameanzishwa Kata.

(2) Ngazi ya Kata kwa shughuli za chama itatumika kwa Tanzania Bara tu.

(3) Kutakuwa na vikao vifuatavyo katika kila Kata

a. Mkutano Mkuu wa Kata;

b. Kamati ya Uongozi ya Kata na;

c. Secretariat ya Kata.

*Viongozi Wakuu wa ACT Kata*

30. Viongozi wakuu wa ACT Kata watakuwa wafuatao:-

a. Mwenyekiti wa ACT Kata;

b. Katibu wa ACT Kata.

*Mkutano Mkuu wa ACT Kata*

31. Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa ACT Kata ambao utakutana mara mbili (2) kwa mwaka. Pale itapotokea dharura unaweza kuitishwa wakati wowote ule na Kamati ya Uongozi ya ACT Kata.

*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT Kata*

32. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT Kata watakuwa kama wafuatavyo:-

a. Wajumbe wote wa kamati ya uongozi ya Kata;

b. Wenyeviti wote wa ACT Tawi kwenye Kata;

c. Makatibu wote wa ACT Tawi kwenye Kata;
d. Katibu wa Mawasiliano na Uenezi, Katibu wa Uchaguzi na Mweka hazina wa kila ACT Tawi ndani ya Kata;
e. Wenyeviti wote wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee wa matawi kwenye Kata;
f. Makatibu wote wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee wa matawi kwenye Kata;
g. Diwani, Diwani wa Viti Maalumu, Mbunge, Mbunge wa Viti Maalum, Mwakilishi na Mwakilishi wa Viti Maalum anayeishi katika Kata/Wadi husika.
h. Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa wanaotokana na Chama kwenye Kata;
i. Wawakilishi wanne wa kila Tawi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa ACT Tawi.

*Kazi na Wajibu wa Mkutano Mkuu wa ACT Kata*

33. Kazi na Wajibu wa Mkutano Mkuu wa ACT Kata utakuwa ufuatao:-

a. Kuchagua viongozi wa ACT Kata kama walivyoorodheshwa kwenye Ibara ya 32(a)-(f) isipokuwa viongozi wa Ngome ambao watachaguliwa kwa mujibu wa miongozo ya Ngome zao;
b. Kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea Udiwani katika Kata husika kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa na Kanuni na miongozo ya Chama.
c. Kujadili taarifa za Kamati ya Uongozi ya Kata na kutoa maamuzi au maelekezo kwa utekelezaji;
d. Kupokea maamuzi na maagizo ya vikao vya juu na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Kamati ya Uongozi;
e. Kuzingatia, kujadili na kuweka miongozo ya utekelezaji wa Falsafa, Itikadi, Misingi na Sera za Chama katika Kata;
f. Kujadili na kutoa mapendekezo kwa ngazi za juu

kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayojitokeza katika Kata, ambayo yanahitaji hatua za kichama ngazi za juu;

g. Kuidhinisha Programu ya Chama katika Kata;

h. Kuchagua wajumbe wawili; mmoja akiwa ni mwanamke, watakaoingia katika Mkutano Mkuu wa Jimbo.

i. Kuchagua wajumbe wa Kamati ya Maadili ya Kata;

j. Kujadili taarifa za utendaji wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee katika Kata.

*Kamati ya Uongozi ya ACT Kata*

34. Kutakuwa na Kamati ya Uongozi ya ACT Kata itakayokutana angalau mara moja kwa kila mwezi, isipokuwa pale itakapotokea haja ya dharura na ya ulazima itaweza kukutana wakati wowote ikiwa Mwenyekiti wa Kata kwa kushauriana na Katibu wa Kata ataamua hivyo.

*Wajumbe wa Kamati Uongozi ya ACT Kata*

35. Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya ACT Kata watakuwa wafuatao:-

a. Mwenyekiti wa ACT Kata;

b. Katibu wa ACT Kata;

c. Katibu Mwenezi wa ACT Kata;

d. Katibu wa Mipango na Chaguzi wa ACT Kata;

e. Mweka hazina wa ACT Kata;

f. Wenyeviti wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee ngazi ya ACT Kata;

g. Wajumbe wanne wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa ACT Kata;

h. Diwani wa kuchaguliwa na wa viti maalum wanaotokana na Chama kwenye Kata husika;

i. Wawakilishi watatu (angalau mmoja awe mwanamke kama yupo) wa wenyeviti wa Mitaa, vijiji na vitongoji na wajumbe wa serikali na kamati za vijiji/mitaa.

*Kazi za Kamati*

36. Kazi za Kamati ya Uongozi ya ACT Kata zitakuwa zifuatazo: -

*ya Uongozi ya ACT Kata*

a. Kupokea na kujadili majina ya wagombea wa Chama katika uchaguzi wa Madiwani na kupeleka kwa Mkutano Mkuu wa Kata kufanyiwa uteuzi;
b. Kuandaa Mkutano Mkuu wa ACT Kata na ajenda zake;
c. Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Chama katika ACT Kata;
d. Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa Chama katika matawi;
e. Kuandaa mikakati na kusimamia kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali ndani ya Kati;
f. Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Falsafa, Itikadi, Misingi na Sera za Chama;
g. Kutekeleza maamuzi ya vikao vya juu vya Chama;
h. Kuweka kumbukumbu sahihi za Uanachama katika rejesta ya wanachama kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni za Chama;
i. Kuandaa taarifa mbali mbali za Chama za ACT Kata na kuziwasilisha kwenye ngazi ya ACT Jimbo kwa mujibu wa Kanuni za Chama;
j. Kuhifadhi kumbukumbu za vikao na nyaraka nyingine za mawasiliano katika Chama;
k. Kufuatilia utendaji kazi wa viongozi wa kiserikali katika Kata waliotokana na Chama na kutoa ushauri au maelekezo kwa kadri inavyowezekana;
l. Kusimamia na kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya ACT Kata husika;
m. Kufuatilia utendaji na utekelezaji wa maelekezo ya Chama kwa wawakilishi wa Chama katika mabaraza ya Serikali za Mitaa;
n. Kutoa msaada kila inapobidi kwa viongozi na wawakilishi wa Chama katika mabaraza ya Serikali za Mitaa;

o. Kutayarisha na kusimamia programu za Chama katika ngazi husika;
p. Kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa maadili ya Chama katika ngazi husika;
q. Kusimamia utendaji wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee katika ACT Kata.

*Sekretarieti ya ACT Kata*

37. (1) Kutakuwa na Sekretarieti ya ACT Kata itakayokutana angalau mara moja kwa kila mwezi, isipokuwa pale itakapotokea haja ya dharura na ya ulazima itaweza kukutana wakati wowote ikiwa Mwenyekiti wa Sekretarieti kwa kushauriana na Katibu wa Sekretarieti ataamua hivyo.

(2) Wajumbe wa Sekretarieti ya ACT Kata watakuwa wafuatao:-

a. Katibu wa ACT Kata atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti;
b. Katibu wa Mawasiliano na Uenezi wa ACT Kata atakuwa Katibu wa Sekretarieti;
c. Mweka hazina wa ACT Kata;
d. Katibu Mipango na Chaguzi wa ACT Kata;
e. Makatibu wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee kwenye Kata.

*Kazi za Sekretarieti ya ACT Kata*

38. Kazi za Sekretarieti ya ACT Kata zitakuwa kama zifuatazo:-

a. Kuandaa Kikao cha Kamati ya Uongozi ya ACT Kata na ajenda zake;
b. Kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Chama katika ACT Kata;
c. Kuandaa mikakati na kuishauri Kamati ya Uongozi ya Kata juu ya kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali;
d. Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Falsafa, Itikadi, Misingi na Sera za Chama;
e. Kutekeleza maamuzi ya vikao vya ACT Kata na vikao vya ngazi za juu vya Chama;

f. Kuweka kumbukumbu sahihi za wanachama katika madaftari ya wanachama kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni za Chama;
g. Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama katika ACT Tawi na kuziwasilisha kwenye ngazi za juu kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

*Kazi za Mwenyekiti wa ACT Kata*

39. Kazi za Mwenyekiti wa Kata/Wadi zitakuwa zifuatazo:-

a. Atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo yote ya Chama katika Kata yake;
b. Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Chama wa ACT Kata na Kamati ya Uongozi ya ACT Kata;
c. Katika Mikutano anayoiongoza, zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa Chama wa ACT Kata pia atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana;
d. Atakuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa Chama katika Kata;
e. Atahakikisha Chama kinashinda uchaguzi wa Udiwani na kupata kura nyingi za Urais na Ubunge katika Kata yake.

*Kazi za Katibu wa ACT Kata*

40. Kazi za Katibu wa ACT Kata zitakuwa zifuatazo:-

a. Atakuwa Katibu wa vikao vyote vya kikatiba vya Chama katika ACT Kata;
b. Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Chama katika Kata;
c. Atakuwa ndiye Mkuu wa mipango ya Chama katika Kata;
d. Atatunza orodha ya Matawi pamoja na wanachama waliopo kwa kila Tawi lililoko katika Kata yake;
e. Atatunza kumbukumbu za mali za Chama zisizohamishika na zinazohamishika zilizopo katika au chini ya ofisi ya Chama ya Kata hiyo;
f. Atawajibika na kutoa taarifa za kila mwezi kuhusu

utendaji wa shughuli za Chama katika Kata kwa ngazi ya ACT Jimbo.

g. Atakuwa ndiye mdhibiti Mkuu wa mali za Chama katika Kata;

h. Atawajibika kuandaa na kuitisha mikutano yote ya vikao halali vya Chama vya Kata kwa maelekezo ya Sekretarieti na Kamati ya Uongozi na kwa kushauriana na Mwenyekiti wake wa Kata;

i. Atafuatilia na kuratibu masuala ya usalama wa Chama katika Kata yake;

j. Atahakikisha Chama kinashinda ngazi zote za Udiwani na kupata kura nyingi za Urais, Ubunge na Uwakilishi;

k. Atafanya kazi yoyote itakayokuwa imetajwa pengine popote katika Katiba hii.

*Kazi ya Mweka hazina wa ACT Kata*

41. Kazi ya Mweka hazina wa ACT Kata/Wadi zitakuwa zifuatazo:-

a. Kutunza mali, fedha za Chama na vitabu vya mahesabu yote ya fedha katika Kata na kuyaweka tayari kwa ajili ya ukaguzi wa ndani ya Chama wakati wote.

b. Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumzi ya kila mwaka ya Chama katika Kata;

c. Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya Kata na ngazi ya juu;

d. Kubuni miradi ya uchumi katika Kata na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya Chama vya ngazi ya ACT Kata na ngazi za juu;

e. Kukusanya mapato ya Chama na kufanya malipo yote katika Kata yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha na taratibu nyengine za Chama kama zitakazotungwa na Kamati Kuu ya Taifa na kuidhinishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa;

f. Kufuatilia ukusanyaji wa mapato yote katika Matawi yaliyomo katika ACT Kata.

## SEHEMU YA NNE

## NGAZI YA JIMBO

*ACT Jimbo na vikao vyake*

42 (1) Kwa mujibu wa Katiba hii Jimbo ni eneo la Uchaguzi kama lilivyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar au Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumchagua Mjumbe wa Baraza la wawakilishi au Mbunge.

(2) ACT Jimbo itakuwa na Vikao vifuatavyo:-

a. Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo
b. Kamati ya Uongozi ya ACT Jimbo na
c. Sekretarieti ya ACT Jimbo

*Viongozi wa ACT Jimbo*

43 Kutakuwa na viongozi wafuatao katika ACT Jimbo:

a. Mwenyekiti wa ACT Jimbo;
b. Katibu wa ACT Jimbo;
c. Katibu wa Mawasiliano na Uenezi wa ACT Jimbo;
d. Mweka Hazina wa Jimbo;
e. Katibu Mipango na Chaguzi ACT Jimbo;
f. Wenyeviti wa Ngome katika ACT Jimbo;
g. Makatibu wa Ngome katika ACT Jimbo; na
h. Wajumbe wanne wa kuchaguliwa wa Kamati ya Uongozi ACT Jimbo watakaochaguliwa na mkutano mkuu wa ACT Jimbo, wanaume wawili na wanawake wawili;
i. Wabunge na Wawakilishi waishio katika Jimbo hilo wanaotokana na Chama.

*Mkutano Mkuu wa Jimbo*

44. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo ambao utakutana katika vikao vya kawaida mara mbili kwa mwaka.

(2) Kamati ya uongozi ya Jimbo inaweza ikiona kuna umuhimu huo kuitisha Mkutano Mkuu wa dharura wakati wowote ule.

*Wajumbe wa Mkutano Mkuu ACT Jimbo*

45. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo watakuwa wafuatao: -

a. Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya ACT Jimbo;
b. Wenyeviti wote wa Kata/Tawi katika Jimbo;
c. Makatibu wote wa Kata/Tawi katika Jimbo;

d. Makatibu wa Uenezi, Makatibu wa Mipango na Waweka hazina wote wa Kata/Tawi katika Jimbo
e. Wenyeviti wa Ngome zote za Kata/Tawi katika Jimbo;
f. Makatibu wa Ngome zote za Kata/Tawi katika Jimbo;
g. Madiwani na Madiwani wa Viti maalum wanaotokana na Chama katika Jimbo;
h. Wabunge, Wawakilishi, Wabunge na Wawakilishi wa Viti Maalum wanaoishi katika Jimbo hilo na ambao wanatokana na Chama;
i. Wajumbe wawili; mmoja akiwa ni mwanamke, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata/Tawi.

*Kazi za Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo*

46. Kazi za Mkutano Mkuu wa ACT Jimbo zitakuwa zifuatazo:-

a. Kuchagua Viongozi wote wa ACT Jimbo waliotajwa katika ibara ya 43 isipokuwa:-
   i. Katibu wa ACT Jimbo ambaye atapigiwa kura kwa kupendekezwa kwa Sekretarieti ya Kamati Kuu ambayo ndiyo itafanya uteuzi wa mwisho.
   ii. Viongozi wa Ngome zote za Chama ambao watateuliwa kwa mujibu wa taratibu na kanuni za Ngome hizo
   iii. Wajumbe wa Baraza la Wawakillishi, Wabunge, Madiwani ambao utaratibu wao wa kuchaguliwa umewekwa wazi ndani ya Kanuni zilizotungwa kwa ajili hio.
b. Bila kuathiri kipengele cha (a) hapo juu, viongozi wa ngome zote watachaguliwa kwa mujibu wa miongozo ya ngome husika;
c. Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utendaji na mapato na matumizi ya ACT Jimbo;
d. Kupokea na kuzingatia mikakati ya ushindi wa Chama katika chaguzi za kiserikali ndani ya ACT Jimbo;
e. Kuzingatia na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Kamati ya Uongozi ya ACT Jimbo juu ya maamuzi na maagizo ya vikao vya juu;
f. Kujadili taarifa za Kamati ya Uongozi ya Jimbo na kutoa maamuzi au maelekezo kwa utekelezaji;

g. Kujadili na kuweka miongozo ya utekelezaji wa Falsafa, Itikadi, Misingi na Sera za Chama katika ACT Jimbo;
h. Kutoa mwongozo na maelekezo kwa wawakilishi wa Chama katika vyombo vya maamuzi vya kiserikali;
i. Kuzingatia na kutoa mapendekezo kwa ngazi za juu, kuhusu masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayojitokeza katika Jimbo na yanayohitaji hatua za kichama ngazi za juu;
j. Kuidhinisha Programu ya Chama katika Jimbo;
k. Kupiga Kura ya maoni ya wagombea wa Ubunge/Uwakilishi na Ubunge na Uwakilishi wa Viti Maalum katika Jimbo husika na kuwasilisha matokeo hayo kwa Kamati Kuu ya Taifa itakayofanya uteuzi wa mwisho.
l. Kupiga kura ya maoni ya Udiwani Viti Maalum katika Jimbo husika kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Kanuni za Chama na kuwasilisha matokeo hayo kwa kamati ya Uongozi ya Mkoa husika kwa uteuzi wa mwisho.
m. Kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea Udiwani wa Wadi zote katika Jimbo husika kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Kanuni na miongozo ya Chama, kwa upande wa Zanzibar.
n. Kuchagua wajumbe wanne; wawili wakiwa ni wanawake, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa.

*Kamati ya Uongozi ya ACT Jimbo na wajumbe wake*

47. (1) Kutakuwa na kamati ya uongozi ya ACT Jimbo itakayokutana kwa vikao vya kawaida angalau mara moja kila mwezi isipokuwa pale itapotokea haja ya dharura ambapo inaweza kukutana wakati wowote ule kama itakavyoamuliwa na Mwenyekiti wa Jimbo kwa kushauriana na Katibu wa Jimbo

(2) Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya ACT Jimbo watakuwa wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Jimbo;
(b) Katibu wa Jimbo;
(c) Katibu wa Mawasiliano na Uenezi wa Jimbo;
(d) Mweka Hazina wa Jimbo;

(e) Katibu Mipango na Chaguzi Jimbo;
(f) Wenyeviti wa Ngome katika Jimbo;
(g) Makatibu wa Ngome katika Jimbo;
(h) Wajumbe wanne wa kuchaguliwa wa Kamati ya Uongozi Jimbo;
(i) Mbunge na/au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi katika jimbo husika;
(j) Meya na/au Naibu Meya anayetokana na ACT ikiwa anaishi ndani jimbo husika;
(k) Mwakilishi wa Madiwani wote wanaotokana na ACT katika jimbo
(l) Wenyeviti na Makatibu wa Kamati mbalimbali zilizoundwa katika ngazi ya jimbo;
(m) Wajumbe wote wa Kamati Kuu wanaoishi katika Jimbo watakaoingia kama waalikwa lakini watakuwa hawana haki ya kupiga kura.

*Kazi za kamati ya Uongozi ya ACT jimbo*

48. Kamati ya uongozi ya ACT Jimbo itakuwa na kazi zifuatazo :-

(a) Kuandaa ajenda za Mkutano Mkuu wa Jimbo;
(b) Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Chama katika Jimbo;
(c) Kusimamia misingi mikuu ya ACT katika jimbo husika;
(d) Kusimamia uchaguzi wa ndani ya chama katika kata/wadi kwa upande wa Bara na uchaguzi wa matawi kwa upande wa Zanzibar;
(e) Kupanga mipango ya kampeni za uchaguzi katika jimbo;
(f) Kuhakikisha chama kinaenea kwenye jimbo lote;
(g) Kupanga na kuandaa mkutano mkuu wa Chama jimbo;
(h) Kuunda Kamati ndogo kadri itakavyoona inafaa; na
(i) Kujaza kwa muda nafasi za uongozi zilizowazi katika jimbo.

*Sekretarieti ya Jimbo*

49. Kutakuwa na Sekretarieti ya Jimbo itakayokutana angalau mara moja kila wiki ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Katibu wa Jimbo ambae atakuwa Mwenyekiti;
(b) Katibu wa Mawasiliano na Uenezi ambaye atakuwa ni

Katibu;
(c) Katibu wa Mipango na Chaguzi wa Jimbo;
(d) Katibu wa kila Ngome wa Jimbo;
(e) Mweka hazina wa Jimbo;
(f) Makatibu wa Kamati mbalimbali katika Jimbo;

(2) Kazi za Sekretarieti ya Jimbo zitakuwa kama ifuatavyo:-

a. Kupokea taarifa ya majina ya wagombea udiwani katika Kata zilizo ndani ya Jimbo na kura za maoni walizopigiwa;
b. Kuandaa kikao cha Kamati ya Uongozi ya Jimbo na ajenda zake;
c. Kuandaa mikakati na kuendesha shughuli za kila siku za Chama katika Jimbo;
d. Kuandaa mikakati itakayopitishwa na Kamati ya Uongozi ya Jimbo kwa ajili ya kusimamia kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali;
e. Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza Falsafa, Itikadi, Misingi na Sera za Chama;
f. Kutekeleza maamuzi ya vikao vya Kamati ya Uongozi na Mkutano mkuu Jimbo;
g. Kuweka kumbukumbu sahihi za wanachama kwa mujibu wa Kanuni za Chama;
h. Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama katika Jimbo na kuziwasilisha kwenye ngazi za juu kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni za Chama;
i. Kuweka kumbukumbu za vikao na nyaraka nyingine za mawasiliano katika Chama;
j. Kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya Jimbo;
k. Kazi nyingine zozote watakazoagizwa na Kamati ya Uongozi ya Jimbo.

*Viongozi Wakuu wa ACT Jimbo*

50. Kutakuwa na viongozi wakuu wafuatao katika Jimbo:-

(a) Mwenyekiti wa ACT Jimbo
(b) Katibu wa ACT Jimbo

*Kazi za Mwenyekiti*

51. Mwenyekiti wa ACT Jimbo atakuwa na kazi zifuatazo:-

a. Atakuwa na wajibu wa kusimamia mambo yote ya Chama katika Jimbo;
b. Atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa mikakati ya ushindi wa Chama katika chaguzi za serikali ndani ya Jimbo, na utendaji wake utapimwa kutokana na, pamoja na mambo mengine, ufanisi wa Chama katika chaguzi za kiserikali ndani ya Jimbo;
c. Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu na Kamati ya Uongozi ya Jimbo;
d. Katika mikutano anayoiongoza, zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa Chama wa Jimbo atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana;
e. Atakuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa shughuli za kila siku za Chama katika Jimbo; na
f. Atahakikisha chama kinashinda uchaguzi wa Uwakilishi na Ubunge na kupata kura nyingi za Urais wa Jamhuri ya Muungano na Urais wa Zanzibar.

*Kazi za Katibu wa ACT Jimbo*

52 Katibu wa ACT Jimbo atakuwa na kazi zifuatazo:

a. Atakuwa Katibu wa mikutano na vikao vya Kamati ya Uongozi na Mkutano Mkuu wa Jimbo;
b. Atakuwa mwenyekiti wa vikao vya Sekretarieti ya Jimbo;
c. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Chama katika Jimbo na atafanya kazi chini ya Kamati ya uongozi ya Jimbo;
d. Atakuwa Mkuu wa mipango ya Chama katika Jimbo;
e. Ataitisha na kuongoza vikao vya wajumbe wa Sekretarieti katika Jimbo kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa ajenda ya vikao vya Jimbo na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya Chama;
f. Ataitisha vikao vya Kamati ya Uongozi ya Jimbo na Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa maelekezo ya Sekretarieti na Kamati ya Uongozi kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Jimbo;
g. Atatunza orodha ya Kata, Matawi na wanachama wa Jimbo lake;

h. Atatunza kumbukumbu za mali za chama zisizohamishika na zinazohamishika zilizopo katika miliki au chini ya ofisi ya Chama ya Jimbo lake;
i. Atakuwa mdhibiti mkuu wa mali za Chama za Jimbo;
j. Atawajibika kutoa taarifa za utendaji wa shughuli za Chama katika Jimbo kila mwezi kwa ngazi ya Mkoa;
k. Atafuatilia na kuratibu masuala ya usalama wa Chama katika Jimbo lake; na
l. Kufanya kazi yoyote itakayokuwa imetajwa penginepo katika Katiba hii.

*Kazi za Mweka hazina wa ACT Jimbo*

53. Mweka hazina wa Jimbo atakuwa na kazi zifuatazo:-

a. Kutunza mali na fedha za Chama na kutayarisha vitabu vya mahesabu na kuviweka tayari kwa ajili ya ukaguzi wa ndani na wa nje wakati wote;
b. Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya Chama katika Jimbo;
c. Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya Jimbo na ngazi ya juu;
d. Kubuni miradi ya uchumi katika Jimbo na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya Chama vya ngazi ya Jimbo na ngazi juu;
e. Kukusanya mapato ya Chama na kufanya malipo yote ya fedha katika Jimbo yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha na taratibu nyingine za Chama;
f. Kufuatilia ukusanyaji wa mapato na malipo ya fedha katika Matawi yaliyomo ndani ya Jimbo hilo.

## SEHEMU YA TANO

## NGAZI YA MKOA

*Muundo wa ACT Mkoa*

54. (1) Ngazi ya Mkoa ni ngazi ileile ya Mkoa wa kiserikali kwa Tanzania Bara na ni sehemu ya eneo la nchi la kiutawala kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa.

(2) Kila Wilaya ya kiutawala ya Zanzibar itachukuliwa

kuwa ni mkoa wa kichama wa ACT.

(3) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza wakati wowote kutangaza Wilaya yoyote ya kiutawala ya Tanzania Bara kuwa ni Mkoa wa kichama kwa Wilaya hiyo.

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza pia ikihisi inafaa na ni kwa maslahi ya chama kuunganisha wilaya mbili au zaidi zilizokamatana kuwa mkoa mmoja wa kichama wa ACT.

(5) Kila wilaya iliyofanywa au wilaya zilizofanywa mkoa nazo zitawajibika kufuata utaratibu ule ule na masharti yale yale yaliyowekwa Kikatiba kuhusu;

(i) Vikao
(ii) Mikutano
(iii) Viongozi
(iv) Kazi na majukumu yao yalivyo katika mkoa.

(6) Vikao vya Mkoa ni pamoja na:-

a. Mkutano Mkuu wa Mkoa
b. Kamati ya Uongozi na
c. Sekretarieti ya Mkoa

(7) Viongozi wa ACT Mkoa ni:-

a. Mwenyekiti wa ACT Mkoa;
b. Katibu wa ACT Mkoa;
c. Mweka hazina wa ACT Mkoa;
d. Katibu wa Mawasiliano na Uenezi wa ACT Mkoa;
e. Katibu wa Mipango na Chaguzi wa ACT Mkoa;
f. Wenyeviti wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee wa ACT Mkoa watakaochaguliwa kwa mujibu wa utaratibu na kanuni za uchaguzi wa Ngome husika;
g. Wajumbe wanne wa kuchaguliwa wa Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa watakaochaguliwa na Mkutano mkuu wa Mkoa, wanaume wawili na wanawake wawili;

h. Wawakilishi na Wabunge wote wa Mkoa husika.

*Mkutano Mkuu wa ACT Mkoa*

55. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa ACT Mkoa utakaofanyika mara moja kwa mwaka na kwamba pale ambapo patakuwa na haja ya muhimu na dharura basi Mkutano Mkuu wa dharura utaitishwa baada ya Mwenyekiti wa Mkoa kushauriana na Katibu wa Mkoa.

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa ni hawa wafuatao:-

a. Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa;
b. Wenyeviti na Makatibu wa majimbo yote yaliyomo kwenye Mkoa;
c. Makatibu wa uenezi, mipango na waweka hazina wa majimbo yote yaliyomo kwenye mkoa;
d. Wenyeviti na Makatibu wa Ngome wa Majimbo yaliyomo katika mkoa;
e. Wajumbe wanne; wawili wakiwa ni wanawake, waliochaguliwa na mikutano mikuu ya majimbo yaliyomo katika mkoa husika.
f. Wabunge, wawakillishi, wabunge na wawakillishi wa viti maalum wanaotokana na Chama kwenye Mkoa husika;
g. Madiwani na madiwani Viti Maalum wote watokanao na Chama katika Mkoa husika;
h. Wajumbe wa Kamati Kuu wanaoishi katika Mkoa husika.

*Kazi za Mkutano Mkuu wa ACT Mkoa*

56. Kazi za Mkutano Mkuu wa ACT Mkoa zitakuwa zifuatazo:-

a. Kuchagua Viongozi wa Mkoa waliotajwa katika Ibara ndogo ya 54 (7) (a) – (e) na (g) hapo juu, isipokuwa Katibu wa Mkoa atapigiwa kura kwa kupendekezwa kwa Kamati Kuu ambayo ndio itafanya uteuzi wa mwisho;
b. Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya utendaji na taarifa ya mapato na matumizi ya Mkoa;
c. Kupokea na kuzingatia mikakati ya ushindi wa Chama katika chaguzi za kiserikali ndani ya Mkoa;
d. Kuzingatia na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Kamati

ya Uongozi ya Mkoa juu ya maamuzi na maagizo ya vikao vya juu;

e. Kujadili taarifa za Kamati ya Uongozi ya Mkoa na kutoa maamuzi au maelekezo kwa utekelezaji;
f. Kujadili na kuweka miongozo ya utekelezaji wa Itikadi, Falsafa, Misingi na Sera za Chama katika Mkoa;
g. Kutoa mwongozo na maelekezo kwa wawakilishi wa Chama katika vyombo vya maamuzi vya kiserikali kwa mambo yanayohitaji msimamo wa chama kimkoa;
h. Kuzingatia na kutoa mapendekezo kwa ngazi za juu, juu ya masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayojitokeza katika Mkoa na yanayohitaji hatua za kichama ngazi za juu;
i. Kuidhinisha Programu ya Chama katika Mkoa.

*Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa na Wajumbe wake*

57. (1) Kutakuwa na Kamati ya uongozi ya ACT Mkoa itakayokutana kila baada ya miezi miwili, na inaweza kuitisha kikao cha dharura ikiwa kuna haja na umuhimu wa kufanya hivyo.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa watakuwa ni:-

a. Mwenyekiti wa ACT Mkoa;
b. Katibu wa ACT Mkoa;
c. Katibu wa Mawasiliano na Uenezi wa ACT Mkoa;
d. Mweka Hazina wa ACT Mkoa;
e. Katibu Mipango na Chaguzi wa ACT Mkoa;
f. Wenyeviti wa Ngome katika Mkoa;
g. Makatibu wa Ngome katika Mkoa;
h. Wajumbe wanne wa kuchaguliwa wa Kamati ya Uongozi Mkoa;
i. Wawakilishi wawili wa wabunge, wawakilishi wawili wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wawakilishi wawili wa madiwani katika Mkoa husika;
j. Mwakilishi wa Mameya/Wenyeviti na mwakilishi wa Manaibu Meya/Makamu wenyeviti wa Halmashauri wanaotokana na Chama katika mkoa husika;
k. Wenyeviti na Makatibu wa Kamati mbalimbali zilizoundwa

katika ngazi ya Mkoa; na

l. Mjumbe wa Kamati Kuu anaeishi kwenye Mkoa husika

*Kazi za Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa*

58. Kazi za Kamati ya Uongozi ya ACT Mkoa itakuwa ni :-

a. Kuratibu shughuli za Chama katika Mkoa;
b. Kutoa ushauri na misaada ya kiutendaji kwa uongozi wa ACT Jimbo katika Mkoa;
c. Kuratibu shughuli za kampeni za wagombea Urais, Ubunge na Uwakilishi katika mkoa na mgawanyo wa majukumu kijimbo;
d. Kuratibu na kuunganisha shughuli za Ngome za Chama katika Mkoa;
e. Kuwa kiunganishi cha Chama na shughuli za kiserikali katika Mkoa;
f. Kuratibu na kutoa taarifa kwa Chama ngazi ya Taifa juu ya hali ya kisiasa, kijamii na kiutawala ndani ya Mkoa;
g. Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Chama katika Mkoa;
h. Kusimamia misingi mikuu ya Chama katika Mkoa husika;
i. Kusimamia uchaguzi wa ndani ya chama katika Majimbo ya mkoa husika;
j. Kupanga mipango ya kampeni za uchaguzi katika Mkoa;
k. Kuhakikisha chama kinaenea kwenye Mkoa wote;
l. Kupanga na kuandaa mkutano mkuu wa Chama Mkoa na ajenda zake;
m. Kuunda Kamati ndogo kadri itakavyoona inafaa; na
n. Kujaza kwa muda nafasi za uongozi zilizo wazi katika Mkoa.
o. Kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa Udiwani wa Viti Maalum na kuwasilisha taarifa ya majina yanayopendekezwa kwa Mamlaka husika

*Sekretarieti ya ACT Mkoa*

59. (1) Kutakuwa na Sekretarieti ya ACT Mkoa ambayo itafanya vikao vyake mara moja kwa kila mwezi, lakini pia inaweza kukutana kwa dharura au kufanya kikao maalum wakati wowote ule pindi wakiona kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Wajumbe wa Sekretarieti ya Mkoa watakuwa ni:-

(i) Katibu wa Mkoa atakuwa ndiye Mwenyekiti;
(ii) Katibu wa Mawasiliano na Uenezi Mkoa atakuwa ndiye Katibu;
(iii) Mweka Hazina wa Mkoa;
(iv) Katibu wa mMpango na Chaguzi wa Mkoa;
(v) Makatibu wa Ngome za Mkoa; na
(vi) Makatibu wa Kamati mbalimbali zilizoundwa katika Mkoa.

*Kazi za Sekretarieti ya ACT Mkoa*

60. Kazi za Sekretarieti ya Mkoa itakuwa ni:-

(i). Kupokea taarifa ya majina ya wagombea Ubunge na Uwakilishi katika majimbo yaliyo ndani ya Mkoa na kura walizopigiwa za maoni kwa ajili ya kumbukumbu za mkoa husika;
(ii). Kuandaa kikao cha Kamati ya Uongozi ya Mkoa na ajenda zake;
(iii). Kuandaa mikakati na kuendesha shughuli za kila siku za Chama katika Mkoa;
(iv). Kuandaa mikakati itakayopitishwa na Kamati ya Uongozi ya Mkoa kwa ajili ya kusimamia kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali;
(v). Kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama kwa kueneza itikadi, falsafa, sera na madhumuni ya Chama
(vi). Kutekeleza maamuzi ya vikao vya Kamati ya Uongozi na Mkutano Mkuu wa Mkoa;
(vii). Kuweka kumbukumbu sahihi za wanachama katika rejesta ya wanachama kwa mujibu wa Kanuni za Chama;
(viii). Kuandaa taarifa mbalimbali za Chama katika Mkoa na kuziwasilisha kwenye ngazi za juu kwa mujibu wa Kanuni za Chama;
(ix). Kuhifadhi kumbukumbu za vikao na nyaraka nyingine za mawasiliano katika Chama;
(x). Kuweka kumbukumbu za mali, mapato na matumizi ya Mkoa na kazi nyingine zozote watakazoagizwa na

Kamati ya Uongozi ya Mkoa.

*Viongozi wa ACT Mkoa*

61. (1) Kutakuwa na viongozi wafuatao wa Chama katika kila Mkoa:
   (i). Mwenyekiti wa Chama ACT Mkoa; na
   (ii). Katibu wa Chama ACT Mkoa.

(2) Mwenyekiti wa Mkoa atakuwa na majukumu yafuatayo.

*Kazi za Mwenyekiti wa ACT Mkoa*

   (i) Atashughulikia au atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo yote ya Chama katika Mkoa;
   (ii) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Chama wa Mkoa, na Kamati ya Uongozi ya Mkoa;
   (iii) Katika mikutano anayoiongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa Chama wa mkoa atakuwa pia na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana; na
   (iv) Atakuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa Chama wa Mkoa.

(3) Kazi za Katibu wa Chama wa Mkoa:

*Kazi za Katibu wa ACT Mkoa*

a. Atakuwa mtendaji mkuu wa shughuli zote za Chama katika mkoa na atafanya kazi chini ya uongozi wa Kamati ya Uongozi ya Chama mkoa;
b. Atakuwa msimamizi mkuu wa mipango ya Chama katika Mkoa;
c. Ataitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Chama katika mkoa kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati ya Uongozi ya Mkoa na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya Chama;
d. Kutunza orodha ya Majimbo, Kata, Matawi, na wanachama wa mkoa wake;
e. Kutunza kumbukumbu za mali za Chama zisizohamishika na zinazohamishika zilizopo katika miliki au chini ya ofisi ya Chama ya mkoa huo;
f. Atakuwa mdhibiti mkuu wa mali za Chama wa mkoa;
g. Atawajibika kutoa taarifa za kila mwezi kuhusu utendaji wa shughuli za Chama katika mkoa kwa ngazi za juu pale inapohitajika.

h. Atakuwa na wajibu wa kuandaa na kuitisha mikutano yote ya vikao vya Chama mkoa kwa maelekezo ya Sekretarieti na Kamati ya Uongozi Mkoa kwa kushauriana na Mwenyekiti wake;
i. Atafuatilia na kuratibu masuala ya usalama wa Chama katika mkoa wake; na
j. Atafanya kazi yoyote itakayokuwa imetajwa penginepo katika Katiba hii au ile atakayopewa na ngazi za juu za Chama.

(4) Mweka hazina wa Mkoa atakuwa na majukumu yafuatayo :-

*Kazi za Mwekahazina wa ACT Mkoa*

a. Kutunza mali na fedha za Chama na kutayarisha madaftari ya mahesabu na kuyaweka tayari kwa ajili ya ukaguzi wa ndani na wa nje wakati wote
b. Kuandaa mapendelezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya Chama katika Mkoa
c. Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya Taifa
d. Kubuni miradi ya uchumi katika Mkoa na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya juu
e. Kufuatilia ukusanyaji wa mapato na malipo ya fedha katika majimbo yaliyomo ndani ya Mkoa huo
f. Kufanya shughuli nyengine zozote za ukusanyaji wa mapato pamoja na kufanya malipo yaliyoidhinishwa kwa kufuata masharti ya katiba hii na masharti ya Kanuni za fedha zilizoidhinishwa na vikao vya juu.

## SEHEMU YA SITA

## WARATIBU WA CHAMA

*Waratibu wa Chama*

62. (1) Kutakuwa na Waratibu wa Chama ambao watasimamia shughuli za Chama na pia kuhakikisha uhai wa Chama katika eneo ambalo mratibu huyo amepangiwa.

(2) Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli za Chama katika maeneo husika kutakuwa na Waratibu katika ngazi ya kanda na eneo.

(3) Kwa madhumuni ya Ibara ya 62 (2) Kanda ina maana ya eneo lolote lile ambalo Halmashauri Kuu ya Taifa imelitaja chini ya Ibara ya 2(3) na (4) cha Katiba hii.

*Liwali wa Chama wa eneo*

63. (1) Kutakuwa na Mratibu wa Chama wa eneno, ambaye kwa madhumuni ya Ibara hii atajulikana kama Liwali atakayewawakilisha wanachama katika vikundi vifuatavyo:-

(a) Katika kila nyumba ishirini katika Mtaa, Kijiji/Kitongoji;
(b) Kwenye mkusanyiko wa kawaida wa wananchi kama masoko, mabaraza, vituo vya mabasi na taxi na kadhalika; au
(c) Mahali pengine popote ambapo Kamati ya Uongozi ya Tawi itaamua;

(2) Liwali wa Chama atateuliwa na Kamati ya Uongozi ya Tawi baada ya kushauriana na wanachama wa eneo linalohusika.

*Kazi za Liwali wa Chama wa eneno*

64. Liwali wa eneo atakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea maagizo kutoka Tawini na kuyafikisha kwa wanachama wa eneo lake;
(b) Kusimamia uhai wa Chama katika eneo lake;
(c) Kutayarisha na kuhifadhi Daftari la wanachama katika eneo lake;

(d) Kuhamasisha wanachama kushiriki katika shughuli za Chama au Ngome za Chama katika eneo lake;
(e) Kubaini vivutio vitakavyowavutia wananchi wengi kujiunga na Chama ikiwa ni pamoja na vikundi vitakavyojishughulisha na miradi ya kiuchumi, michezo mbali mbali inayopendwa na jamii ya eneo hilo;
(f) Kushawishi wananchi katika eleo lake kuwapigia kura wagombea wa Chama katika uchaguzi wa kiserikali unaohusisha vyama vyingine vya siasa au kuwashawishi wanachama kwa kuwapa msimamo wa Chama katika kura ya maoni na kura nyingine zozote zilizokubaliwa na Chama;
(g) Kufanya kazi nyingine yoyote atakayopewa na uongozi wa Tawi au vikao vya juu.

*Mratibu wa Kanda*

65. Mratibu wa Chama wa Kanda ambaye kwa wadhifa wake huo atakuwa pia ni mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa, atateuliwa na Halmashauri Kuu ya Chama baada ya kupata mapendekezo ya:-

(a) Kamati Maalum ya Kamati Kuu ya Tazania Bara kwa Mratibu wa Kanda zilizoko Tanzania Bara; na
(b) Kamati Maalum ya Kamati Kuu ya Zanzibar kwa Mratibu wa Kanda zilizoko Zanzibar.

*Kazi za Mratibu wa Kanda*

66. Kazi za Mratibu wa Kanda zitakuwa ni:-

(a) Kupokea maagizo kutoka kwa ngazi ya Taifa na kuyafikisha pamoja na kuyafanyia kazi katika Kanda yake.
(b) Kusimamia uhai wa Chama katika Kanda yake;
(c) Kuwa na taarifa kamili ya kila Tawi, Kata Wadi, Jimbo na Mkoa iliyoko katika Kanda yake;
(d) Kuhamasisha wanachama wa kanda yake kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Chama na Ngome zake;
(e) Kushirikiana na Uongozi wa kila Mkoa, Jimbo, Kata zilizopo katika kanda yake na kubuni vivutio vitakavyo wahamasisha wanachama walio katika maeneo hayo kwa kufanya miradi mbali mbali itakayowasaidia

wanachama hao;

(f) Kwa kushirikiana na uongozi wa Tawi, Kata, Jimbo na Mkoa kuwashawishi wanachama na wananchi kwa ujumla wake waliyopo ndani ya eneo lake kuwapigia kura wagombea wa Chama wa ngazi zake katika uchaguzi wa kiserikali unaohusisha vyama vingine vya siasa;

(g) Kuwaelimisha wanachama kuhusu msimamo wa Chama katika uchaguzi wa serikali au jambo jingine lolote ambalo litahitaji maamuzi ya wanachi;

(h) Kuwahamasisha wanachama waliyomo katika kanda yake kuwa na umoja na ushirikiano kwa ajili ya kukijenga vyema Chama na kuonesha taswira nzuri ya Chama;

(i) Kuwa na ushirikiano mazuri na wa karibu kwa Mikoa yake iliyomo ndani ya Kanda yake kwa lengo la kufanikisha mambo yaliyoelezwa katika Ibara ya 66 (a)- (h);

(j) Kufanya kazi nyingine yoyote atakayopewa na vikao vya juu vya Chama.

## SEHEMU YA SABA

## NGAZI YA TAIFA

*ACT Taifa*

67. (1) Eneo la Chama ngazi ya Kitaifa ni eneo lote la Tanzania Bara na Zanzibar kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar na sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi.

(2) Eneo hilo litaundwa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Chama zilizotungwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

*Vikao vya ACT Taifa*

68. Kutakuwa na vikao vifuatavyo vya Chama katika ngazi ya Taifa

(i). Mkutano Mkuu wa Taifa

(ii). Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia Taifa

(iii). Halmashauri Kuu ya Taifa

(iv). Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa
(v). Kamati ya Uongozi ya Taifa
(vi). Sekretarieti ya Kamati Kuu

*Mkutano Mkuu wa ACT Taifa*

69. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Taifa utakaofanyika mara moja kila baada ya miezi sitini (60) na utakuwa ndio chombo kikuu cha Chama chenye maamuzi ya mwisho ya shughuli zote za Chama nchini.

(2) Mkutano Mkuu wa Taifa wa dharura unaweza kuitishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa endapo itatokea haja na sababu muhimu kufanya hivyo.

(3) Kikao cha dharura cha Mkutano Mkuu wa Taifa kitafanyika pale tu zaidi ya nusu ya wajumbe wa Halmashauri Kuu wanaotoka Zanzibar na zaidi ya nusu ya wajumbe wa Halmashauri Kuu wanaotoka Tanzania Bara watatia saini kuitishwa Mkutano huo, na Mkutano Mkuu huo utaitishwa ndani ya siku mia moja na themanini (180) tangu siku lilipopokelewa ombi hili.

(4) Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa halali pale tu zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka Tanzania Bara na zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka Zanzibar watahudhuria.

(5) Maamuzi yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Taifa yatakuwa ni maamuzi halali ikiwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote waliohudhuria watayaunga mkono.

(6) Maamuzi muhimu yatahesabiwa kuwa maamuzi halali ya Mkutano Mkuu wa Taifa ikiwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe kutoka Tanzania Bara waliohudhuria, na zaidi ya theluthi mbilli (2/3) ya wajumbe kutoka Zanzibar waliohudhuria watayaunga mkono maamuzi hayo.

(7) Kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (6) hapo juu maamuzi muhimu ni pamoja na:-
   (a) Kuvunja Chama;
   (b) Kubadilisha jina la Chama;
   (c) Kuunganisha Chama na Chama au vyama vingine vya siasa;
   (d) Kuwasimamisha, kuwaachisha au kuwafukuza uongozi na/au uanachama viongozi wakuu wa kitaifa wa Chama pamoja na viongozi wengine wa kitaifa kama

ilivyoainishwa ndani ya Katiba hii;
(e) Kuwaachisha, kuwafukuza uanachama Rais na/au Makamu Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais na/au Makamu Rais wa Zanzibar anayetokana na Chama;
(f) Kupitisha, kurekebisha au kubadilisha Katiba hii au kifungu chochote cha Katiba hii;
(g) Kupitisha, kurekebisha au kubadilisha Itikadi ya Chama;
(h) Mambo mengine yoyote ambayo Mkutano Mkuu wa Taifa kwa masharti yale yale ya Ibara ndogo ya (6) ya ibara hii utaamua kuwa ni maamuzi muhimu.

*Halmashauri Kuu kuongeza au kurudisha nyuma muda wa kufanya Mkutano Makuu*

70. (1) Pale ambapo wakati wa kufanya Mkutano Mkuu wa Taifa umefika, na kutokana na sababu iliyotokea, haiwezekani kufanyika kwa Mkutano Mkuu kwa kipindi hicho, au Halmashauri Kuu inaona ni vyema Mkutano Mkuu ufanyike mapema zaidi kabla ya tarehe inayofuata ya Mkutano Mkuu mwingine, basi Halmashauri Kuu, kwa azimio watakalolitoa, inaweza kuahirisha au kurudisha nyuma tarehe ya Mkutano huo kwa kipindi kisichozidi miezi sita tokea siku ambayo mkutano huo ulikuwa ufanyike.

(2) Ikiwa Halmashauri Kuu itatoa azimio la kuahirisha Mkutano Mkuu, basi kipindi hicho cha miezi sita kinaweza kuongezwa tena kwa kutumia utaratibu ulioelezwa katika ibara ndogo ya kwanza (1) hapo juu kwa kipindi hicho hicho cha miezi sita tena, na baada ya hapo Mkutano Mkuu huo utalazimika ufanywe na wala hautaongezwa muda mwingine wowote.

(3) Sababu au jambo la dharura kwa maana ya Ibara hii ni pamoja na:-
(i) Kuwepo kwa maradhi ya mlipuko au aina yoyote ya maradhi yaliyotokea nchini ambayo mamlaka ya serikali imepiga marufuku mkusanyiko wa aina yoyote ile;
(ii) Kuwepo na janga lolote lile la kitaifa lilitokea na bado likawa linaendelea;
(iii) Kuwepo na tatizo la upungufu mkubwa wa fedha za kuendeshea Mkutano huo;

(iv) Jambo jingine lolote ambalo Halmashauri Kuu itaona kwa manufaa ya chama ni jambo la dharura la kuweza kuahirisha au kurudisha nyuma tarehe ya Mkutano Mkuu huo hadi siku nyingine.

(4) Pale ambapo Halmashauri Kuu imeamua kuahirisha Mkutano Mkuu na kusogeza mbele au kurudisha nyuma tarehe ya kufanyika kwake, basi Katibu Mkuu atamjulisha Msajili wa Vyama vya Siasa:-

(a). Azimio hilo na kumjuilisha rasmi;
(b). Sababu ambazo zimelazimisha kuahirishwa au kurudishwa nyuma kwa Mkutano Mkuu huo;
(c). Tarehe nyingine iliyopangwa kufanyika Mkutano huo.

*Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa*

71. Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:-

a. Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa;
b. Wenyeviti na Makatibu wa Majimbo;
c. Wawakilishi sita wa Ngome za Chama Taifa kwa wawakilishi wawili kila Ngome;
d. Wawakilishi sita wa wanafunzi wa vyuo vikuu waliochaguliwa na umoja wao kwa mujibu wa Kanuni zitakazowekwa na Ngome ya Vijana, kwa masharti kwamba angalau theluthi moja ya wajumbe hao watakuwa wanawake;
e. Wawakilishi wawili wa wanachama wa ACT Nje watakaochaguliwa na wanachama walio nje ya nchi kwa sharti kwamba angalau mmoja awe mwanamke na kwamba wawakilishi hao ni lazima wawe raia wa Tanzania.
f. Wawakilishi wote wanaotokana na Chama;
g. Wabunge wote wanaotokana na Chama;
h. Wawakilishi kumi (10) wa madiwani waliochaguliwa na Jumuiya zao, watano wakitokea Zanzibar na Watano wakitokea Tanzania Bara na ambao angalau theluthi moja wakiwa wanawake.

*Kazi za Mkutano Mkuu Taifa*

72. (1) Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na kazi na wajibu ufuatao:-

a. Kuchagua Kiongozi wa Chama;
b. Kuchagua Mwenyekiti wa Chama Taifa;
c. Kuchagua Makamu Mwenyekiti Bara wa Chama Taifa;
d. Kuchagua Makamu Mwenyekiti Zanzibar wa Chama Taifa;
e. Kujadili taarifa za Halmashauri Kuu na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji;
f. Kuteua Mgombea wa Urais na Mgombea mwenza kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgombea Urais wa Zanzibar;
g. Kujadili na kuridhia Itikadi, Falsafa, Misingi na Sera za Chama kisha kuweka mikakati na miongozo ya utekelezaji;
h. Kujadili na kuridhia programu ya Chama kwa kuzingatia mapendekezo ya Halmashauri Kuu;
i. Kupokea na kujadili taarifa ya Bodi ya Wadhamini ya Chama juu ya mali na raslimali za Chama;
j. Kuipokea Ilani (Manifesto) ya Chama kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu na kutoa maelekezo yake ikiwa italazimu kufanya hivyo;
k. Kupokea na kujadili ripoti ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama kutoka kwa Waziri Mkuu wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar wanaotokana na Chama;
l. Kupokea, kujadili na kuridhia au kurekebisha ripoti ya fedha pamoja na shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano iliopita;
m. Kuchagua wajumbe kumi na watano wa Halmashauri Kuu Taifa kwa sharti kuwa wajumbe kumi watatoka Tanzania Bara angalau wanne kati yao wakiwa wanawake na wajumbe watano kutoka Zanzibar angalau wawili kati yao wakiwa wanawake.

(2) Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya: -

(i) Taarifa za fedha za kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa pamoja.
(ii) Taarifa za mkaguzi wa nje wa mahesabu ya Chama ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa pamoja.
(iii) Taarifa ya mapato na matumizi ya Chama ya kila

mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa pamoja.

(iv) Mapendekezo ya mipango ya maendeleo ya Chama na Serikali inayoendeshwa na Chama.

(v) Taarifa za utekelezaji wa Itikadi na Sera za Chama kutoka Viongozi wa Chama na Viongozi wa Serikali inayoendeshwa na Chama na viongozi wa Wabunge na Wawakilishi wa Chama.

(b) Kutunga, kusahihisha au kurekebisha Katiba ya Chama.

(c) Kuthibitisha itikadi na sera za Chama sera nyingine zilizotungwa na Halmashauri Kuu ya Taifa, na kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya taarifa ya utekelezaji wa itikadi na sera hizo.

(d) Kubuni, kufanya tathmini na kutoa maelekezo juu ya mipango ya kukiimarisha Chama nchini kote.

(e) Kujenga udugu wa dhati miongoni mwa watanzania wote pamoja na wananchi wa nchi jirani na nchi nyingine duniani.

(f) Kuthibitisha au kutengua uamuzi wowote uliotolewa na kikao chochote cha chini au kiongozi yeyote wa Chama.

(g) Kupokea Rufaa na kutoa maamuzi ya mwisho juu ya Rufaa hizo kutoka viongozi au wanachama waliochukuliwa hatua za kinidhamu na vikao vya chini, isipokuwa pale ambapo Katiba hii imeelekeza vinginevyo.

(h) Bila ya kuathiri Ibara ya 69(6) na (7) ya Katiba hii kutoa uamuzi wa kubadili jina la Chama, kuunganisha Chama hiki na chama au vyama vingine vya siasa nchini, au hata kukivunja Chama.

(3) (a) Mkutano Mkuu wa Taifa unaweza kuchukua hatua za kinidhamu zikiwemo kumsimamisha au kumfukuza uongozi au uanachama au yote mawili kwa pamoja Kiongozi wa Chama au Kiongozi wa yeyote wa kitaifa wa Chama au Kiongozi yeyote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atokanaye na Chama hiki.

(b) Bila ya kuathiri masharti ya vifungu vingine vyovyote vya Katiba hii Mwanachama mwingine yeyote naye pia anaweza

kuchukuliwa hatua za kinidhamu zilizoelezwa ibara ya 103 (3) ya Katiba hii.

(4) Mkutano Mkuu wa Taifa utaongozwa na Mwenyekiti wa Taifa na asipoweza kuhudhuria kikao hicho basi kitaongozwa na Makamu Mwenyekiti anaetoka upande mwingine wa Muungano na ikiwa Makamu Mwenyekiti huyo naye hataweza kuhudhuria kikao hicho, kikao kitaongozwa na Makamu Mwenyekiti mwingine na ikiwa yeye pia hayupo, kikao kitamchagua mjumbe mmoja wa Mkutano Mkuu wa Taifa mwenye uzoefu mkubwa asiyekuwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu au mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa kuongoza kikao hicho na mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho.

*Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia*

73. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Taifa wa Kidemokrasia (National Democratic Congress) ambao ni Mkutano Mkuu wa wanachama wote wa ACT Wazalendo.

(2) Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia utajumuisha wajumbe wengine wafuatao:-

(i). Wadau wote wenye mahusiano na ACT Wazalendo;

(ii). Wafadhili wa Chama;

(iii). Wananchi wote bila kujali kama ni wanachama au si wanachama wa ACT Wazalendo kwa sharti kuwa Mkutano huu hautojihusisha na itikadi ya mtu kichama au kidini.

(3) (i) Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia utahutubiwa na Kiongozi wa Chama kwa kutoa muelekeo wa kisera wa Chama na pia litakuwa ni jukumu la wanachama wote pamoja na wajumbe wengine wa Mkutano huu kuhoji kazi za Kiongozi wa Chama, utendaji wake na muelekeo wa Chama katika kufanikisha malengo na madhumuni ya Chama.

(ii) Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia pia utajadilli hali ya siasa na uchumi ya Tanzania Bara na Zanzibar, Afrika na Dunia kwa ujumla.

(4) Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia hautakuwa na madaraka yoyote ya maamuzi, isipokuwa Kiongozi wa Chama akiona

umuhimu na kwa maslahi ya Chama, anaweza kuchukua maoni na mapendekezo yaliyofikiwa na kuyapeleka katika vikao vya Chama vyenye madaraka ya maamuzi kwa ajili ya kuchukuliwa hatua zinazofaa.

*Halmashauri Kuu ya ACT Taifa*

74. (1) Kutakuwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa itakayokutana mara mbili kwa mwaka.

(2) Halmashauri Kuu ya Chama inaweza kukutana katika kikao cha dharura wakati wowote ule ikiwa Kamati ya Uongozi Taifa itashauriana na kuona haja na umuhimu wa kuitishwa.

*Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa*

75. (1) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Taifa watakuwa wafuatao:-

(a) Wajumbe wote wa Kamati Kuu;
(b) Wenyeviti wote wa Mikoa;
(c) Makatibu wote wa Mikoa;
(d) Wenyeviti na Makatibu wa Ngome za Chama Taifa;
(e) Wawakilishi sita wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee kwa kila Ngome kuwakilishwa na wajumbe wawili;
(f) Wawakilishi watatu wa wabunge mmoja wao akiwa ni mwanamke na wawakilishi watatu wa Baraza la wawakilishi mmoja wao akiwa ni mwanamke wanaotokana na ACT;
(g) Wawakilishi watatu wa wanafunzi wa elimu ya juu watakaochaguliwa kwa utaratibu utakaoelezwa kwenye Mwongozo wa Ngome ya Vijana mmoja wao akiwa mwanamke;
(h) Wawakilishi watatu wa Madiwani kutoka Tanzania Bara mmoja wao akiwa ni mwanamke na wawili kutoka Zanzibar mmoja wao akiwa mwanamke;
(i) Wajumbe kumi na tano (15), kwa sharti kwamba kumi kutoka Tanzania Bara kati yao angalau wanne (4) watakuwa wanawake, na watano kutoka Zanzibar angalau wawili (2) watakuwa wanawake, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.
(j) Kiongozi wa kambi ya wabunge Bungeni na kiongozi wa

kambi ya wawakilishi Baraza la Wawakilishi wanaotokana na Chama;

(k) Wajumbe watatu walemavu, wawili kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar miongoni mwao akiwemo mwanamke mmoja ambao watateuliwa na Mwenyekiti kwa kushauriana na Makamu wawili wa Mwenyekiti;

(l) Wajumbe watano, watatu kutoka Tanzania Bara mmoja atakuwa mwanamke na wawili kutoka Zanzibar mmoja wao atakuwa mwanamke ambao wote watateulliwa na Mwenyekiti kwa kushauriana na Makamu wake wawili.

(m) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini ya ACT - Wazalendo

(2) Endapo nafasi ya mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile, basi nafasi hiyo itajazwa kwa kuzingatia Katiba hii na Kanuni zinazohusika na nafasi hiyo na kwa vyovyote vile si zaidi ya miezi kumi na mbili tangu nafasi hiyo kuwa wazi.

(3) Maamuzi yote ya Halmashauri Kuu yatafikiwa kwa maafikiano au kutokana na wingi wa kura pale yanapoamuliwa kwa kupiga kura.

(4) Maamuzi muhimu yatahesabiwa kuwa ni halali ikiwa zaidi ya theluthi mbili ya wajumbe kutoka Tanzania Bara na zaidi ya theluthi mbilli ya wajumbe kutoka Zanzibar watayaunga mkono.

(5) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (4) hapo juu maamuzi muhimu yatahusu mambo yale yalioorodheshwa katika kifungu cha 69 (6) na (7) cha Katiba hii kwa kadri yatakavyorekebishwa mara kwa mara.

*Kazi na wajibu wa Halmashauri kuu ya Chama*

76. (1). Halmashauri Kuu ya Chama Taifa itakuwa na kazi na wajibu ufuatao:-

a. Kupendekeza wagombea wa Urais na Umakamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniana na kuwasilisha mapendekezo yake katika Mkutano Mkuu wa Taifa;

b. Kupendekeza wagombea wa Urais wa Zanzibar na kuwasilisha mapendekezo yake katika Mkutano Mkuu wa Taifa;
c. Kuthibitisha Uteuzi wa Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu wa Tanzania Bara na Zanzibar kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa Chama Taifa baada ya kushauriana na Kiongozi wa Chama na Makamu wake wawili;
d. Kuchagua wajumbe kumi kuingia kwenye Kamati Kuu, sita kutoka Tanzania Bara na wanne kutoka Zanzibar;
e. Kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya rufaa za kinidhamu kwa mujibu wa Katiba hii;
f. Kujadili mikakati ya uendeshaji wa shughuli za Chama kwa kipindi cha mwaka uliopita kuifanyia maamuzi panapostahili;
g. Kuthibitisha mikakati na raslimali za kuendesha kampeni za wagombea wa Chama katika chaguzi za Serikali hususani Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa;
h. Kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa ndani ya chama kwa mujibu wa Katiba na kupitisha kalenda ya uchaguzi kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama;
i. Kutunga na kuzifanyia marekebisho Kanuni za uendeshaji wa Chama;
j. Kujadili taarifa za Kamati Kuu na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji;
k. Kusimamia utendaji kazi wa Kamati Kuu;
l. Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu masuala yote ya Katiba ya Chama na mabadiliko yake;
m. Kujadili na kuidhinisha rasimu ya Ilani (Manifesto) ya uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu na uchaguzi wa Serikali za Mitaa na baadaye kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu kwa taarifa;
n. Kuteua Wadhamini wa Chama;
o. Kuthibitisha miongozo ya Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee;
p. Kujadili na kuidhinisha majina ya wagombea wa nafasi za Kiongozi wa Chama, Mwenyekiti na Makamu Wenyeviti wa Chama.
q. Kukuballi au kukataa pendekezo la Mwenyekiti na Kiongozi

wa Chama kuhusu jina la mtu ambaye atamteua kuwa Mshauri Mkuu wa Chama na Mwanasheria Mkuu wa Chama.

(2) Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa na wajibu ufuatao:-

a. Kutoa ufafanuzi wa Itikadi ya Chama iliyobuniwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa;
b. Kutunga sera na Ilani za Uchaguzi za Chama.
c. Kusimamia utekelezaji bora wa maamuzi na maelekezo mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Taifa;
d. Kutoa miongozo na maelekezo ya kisiasa kwa ngazi za chini za Chama katika kuhakikisha utekelezaji bora wa Katiba hii, itikadi ya Chama, falsafa, misingi, maadili na sera za Chama.
e. Kulinda na kuendeleza heshima ya Chama na serikali zote halali za nchi.
f. Kuanzisha, kufuta au kuongeza Idara za Chama za Taifa, na vitengo vya Chama vya mikoa na kuziunganisha au kuzitenganisha inapohitajika pamoja na kupanga majukumu na kazi za Kamati na Vitengo hivyo, ikiwa ni pamoja na kuiongezea, au kuipunguzia majukumu Idara au Kitengo chochote kile.
g. Kujenga na kuimarisha uhusiano mwema na vyama vingine vya siasa vya ndani na nje ya nchi, vinavyofuata na kuzingatia demokrasia ya kweli;
h. Kuhamasisha kuheshimiwa kwa haki za binaadamu na haki za watu kama zilivyotangazwa na Matamko ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika;
i. Kuendeleza amani na utulivu na kupinga vitendo vyovyote vinavyoashiria utawala wa mabavu.
j. Kuzingatia maombi ya vyama vingine vya siasa na, au jumuiya za vyama vya siasa vya ndani na nje ya nchi vitakavyoomba kushirikiana au kujiunga na ACT.
k. Kuandaa ajenda za Mkutano Mkuu wa Taifa.
l. Kuthibitisha Kanuni zote zilizowasilishwa kwake na Kamati Kuu ya Taifa.
m. Kuwachukulia hatua za nidhamu viongozi na wanachama wanaoshutumiwa kwa makosa mbalimbali kwa kufuata masharti ya Katiba hii na Kanuni

zitakazotungwa mara kwa mara kwa mujibu wa Katiba hii.

(3) Katika kusimamia vyema shughuli za utendaji katika Chama, Halmashauri Kuu ya Taifa:-

a. Itafuatilia kwa karibu shughuli zote za Makao Makuu na Ofisi Kuu ya Chama na Kanda na kutoa maelekezo ipasavyo;
b. Itapokea na kujadili taarifa za utendaji kutoka kwa Kamati Kuu ya Taifa, ngazi za Mikoa, Majimbo, Kata na Matawi na kutoa miongozo mbalimbali ya kufanikisha shughuli za Chama nchini kote;
c. Itasimamia na kufuatilia kwa ukaribu kazi za Kamati zote za Chama;
d. Itateua Bodi ya Wadhamini ya Chama.
e. Itateua Mkaguzi wa Ndani wa Mahesabu ya Chama.
f. Itathibitisha Makatibu na Manaibu Makatibu wa Kamati za Chama waliopendekezwa na Katibu Mkuu wa Chama baada ya kushauriana na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.
g. Itahakikisha kwamba alama muhimu za Chama zinasajiliwa kwa mujibu wa sheria.
h. Itahakikisha utekelezaji bora na wa dhati wa masharti yote ya sheria za nchi zinazohusu usajili wa vyama vya siasa, uendeshaji wa vyama vya siasa na mapato na matumizi ya fedha na mali nyingine za Chama.
i. Itapokea mialiko kutoka vyama rafiki vya ndani na nje ya nchi.
j. Itajadili mapendekezo ya mapato na matumizi ya chama yaliyoletwa na Kamati Kuu kwa kuidhinishwa na au kurekebishwa.

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa litaongozwa na Mwenyekiti wa Chama Taifa, na asipoweza kuhudhuria, kikao hicho kitaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama, anayetoka upande tofauti na Mwenyekiti na ikiwa naye hayupo basi Makamu Mwenyekiti aliyepo ataongoza kikao hicho, ikiwa naye pia hayupo basi kitamchagua mjumbe mwingine yeyote

yule asiyekuwa:

a. Katibu Mkuu, au
b. Mjumbe wa Kamati Kuu.

Ili aongoze kikao hicho, na uenyekiti wake wa muda utamaliza mara tu kikao hicho kitapomalizika

*Kuwasimamisha Uongozi na Uanachama*

77. (1) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kuwasimamisha uongozi Viongozi Wakuu wa Chama wa Taifa wafuatao: -

a. Kiongozi wa Chama;
b. Mwenyekiti wa Chama Taifa;
c. Makamu Wenyeviti.
d. Katibu Mkuu

(2) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kuwasimamisha Uanachama Viongozi Wakuu wa Serikali wa Taifa watokanao na Chama wafuatao: -

a. Rais wa Jamhuri ya Muungano.
b. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.
c. Rais wa Zanzibar.
d. Makamu wa Rais wa Zanzibar
e. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

(3) Endapo kiongozi yeyote aliyetajwa katika Ibara ndogo (1) na (2) ya Ibara hii atasimamishwa Uongozi, Halmashauri Kuu ya Taifa italazimika kufikisha mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa, taarifa ya kusimamishwa uongozi au uanacahama kiongozi huyo kwa haraka kama itakavyowezekana, taarifa hiyo, ikieleza sababu za kuchukuliwa kwa hatua hiyo na mapendekezo ya Halmashauri Kuu Taifa, yatafikishwa mbele ya Mkutano Mkuu Taifa ulio mbele lakini kwa vyovyote vile taarifa ifikishwe katika kipindi kisichozidi siku tisini (90) tangu uamuzi huo uchukuliwe.

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya viongozi watokanao na Chama wafuatao: -

(a). Naibu Katibu Mkuu.

(b). Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa.
(c). Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini.
(d). Waziri Mkuu
(e). Kiongozi wa Upinzani Bungeni.
(f). Makamu wa Rais wa Zanzibar
(g). Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi.
(h). Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.
(i). Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.
(j). Mwenyekiti wa Ngome ya Chama.
(k). Katibu wa Ngome ya Chama.
(l). Kiongozi mwengine yeyote wa Chama na Serikali wa ngazi yoyote ile.

(5) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kuchukua hatua za kinidhamu kama zilivyoelezwa chini ya ibara ya 103 (3) ya Katiba dhidi ya kiongozi yeyote alietajwa katika ibara ndogo ya (4) hapo juu.

(6) Endapo Halmashauri Kuu ya Taifa itamvua madaraka mjumbe wa Bodi ya Wadhamini au Naibu Katibu Mkuu, litalazimika kumteua mjumbe mwingine wa Bodi ya Wadhamini au kumchagua Naibu Katibu Mkuu mwingine kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii katika kikao chake kinachofuata ikiwa muhusika hakukata Rufaa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa.

*Kamati Kuu ya Chama Taifa*

78. (1) Kutakuwa na Kamati Kuu ya Chama Taifa ambayo itakutana kwa mara moja kila baada ya miezi mitatu

*Mwenyekiti Taifa kuitisha Kamati Kuu Taifa ya Dharura*

(2) Mwenyekiti wa Taifa akiona kuna haja na umuhimu, kwa kuzingatia maslahi ya Chama anaweza kuitisha kikao cha dharura cha Kamati Kuu baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi Taifa.

(3) Wajumbe wa Kamati Kuu ya Chama Taifa watakuwa wafuatao:-

(i). Kiongozi wa Chama;
(ii). Mwenyekiti wa ACT Taifa;
(iii). Makamu Wenyeviti wa ACT Taifa;

(iv). Katibu Mkuu;
(v). Manaibu Katibu Wakuu;
(vi). Mwanasheria Mkuu wa Chama;
(vii). Mshauri Mkuu wa Chama
(viii). Waratibu wa Kanda wa Chama;
(ix). Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili Taifa;
(x). Makatibu na Naibu Katibu wa Idara za Chama;
(xi). Wajumbe kumi na Tano waliochaguliwa na Halmashauri Kuu kwa kuzingatia kuwa wajumbe kumi watatoka bara ambao angalau watatu (3) watakuwa wanawake, na wajumbe watano (5) watatoka Zanzibar ambao angalau wawili (2) watakuwa wanawake;
(xii). Wajumbe watano walioteuliwa na Kiongozi wa Chama kwa kushauriana na Mwenyekiti kwa mujibu wa Katiba hii;
(xiii). Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Zanzibar au Makamu wa Rais wa Zanzibar aliyetokana na ACT;
(xiv). Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Spika na Naibu Spika wa Baraza la wawakilishi waliotokana na ACT;
(xv). Waziri Mkuu au Kiongozi wa Kambi ya wabunge wanaotokana na ACT katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Kiongozi wa Kambi ya wawakilisi wanaotokana na ACT kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar;
(xvi). Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu wa Bodi ya Wadhamini;
(xvii). Wenyeviti na Makatibu wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee

Kazi za Kamati Kuu Taifa

79. (1) Kazi za Kamati Kuu ya Chama itakuwa ni:

(i). Kuandaa na kutoa Mapendekezo kwa Halmshauri Kuu, Mikakati ya kuendesha shughuli za Chama kwa kila mwaka na kwa kipindi cha miaka mitano;
(ii). Kuandaa na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri Kuu, Mikakati ya kupata rasilimali za kuendesha kampeni za

wagombea wa Chama katika chaguzi za kiserikali;

(iii). Kupitisha ratiba na miongozo ya uteuzi wa wagombea ndani ya chama kwa Chaguzi za kiserikali;

(iv). Kupitia na kutoa kwa Halmashauri Kuu mapendekezo ya haja ya kuzifanyia masahihisho au marekebisho Kanuni za Chama au Katiba ya Chama;

(v). Kujadili taarifa za Sekretarieti ya Kamati Kuu na kutoa maamuzi na maelekezo kwa utekelezaji;

(vi). Kusimamia utendaji kazi wa Sekretarieti ya Kamati Kuu;

(vii). Kuwateua na kuwapangia vituo vya kazi Makatibu wa Majimbo na Mikoa;

(viii). Kumsimamisha Uongozi Katibu au Naibu Katibu wa Idara za Sekretarieti ya Kamati Kuu kwa utovu wa nidhamu au kushindwa kazi na kuitaarifu Halmashauri Kuu ya Taifa kwa uamuzi wa mwisho;

(ix). Kumsimamisha, kumuachisha au kumfukuza uongozi Kiongozi yeyote wa Mkoa, Jimbo, Kata na Wadi kutokana na makosa ya kinidhamu, uchochezi wa migogoro na ubadhirifu wa fedha na mali za Chama au kushindwa kazi;

(x). Kusimamisha, kuiachisha au Kuivunja kazi Kamati ya Uongozi ya Mkoa, Jimbo, Kata, Wadi au Ngome ya Chama kwa kushindwa kufanya kazi za Chama, kushabikia migogoro miongoni mwa viongozi na ubadhirifu wa fedha na mali za chama;

(xi). Kutunga Rasimu ya Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Katiba hii, na kuziwasilisha katika Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kuthibitishwa;

(xii). Kufanya mapitio ya Sera za Chama na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri Kuu kwa kuzingatia matokeo ya Utafiti uliofanywa na Sekretarieti ya Kamati Kuu;

(xiii). Kusimamia utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu;

(xiv). Kuwa kiungo na kudumisha mahusiano mema kati ya Chama na vyama vingine vya siasa nchini, Afrika Mashariki, Afrikla na nchi nyingine duniani;

(xv). Kuteua Kamati au Tume za kushughulikia masuala

maalumu ya kichama kwa muda maalumu;

(xvi). Kuteua wakaguzi wa mahesabu ya Chama kwa kila mwaka;

(xvii). Kuthibitisha uteuzi wa wagombea Uspika na Naibu Spika, Ubunge, Uwakilishi, Ubunge na Uwakilishi wa Viti Maalum;

(xviii). Kuandaa ajenda za Halmashauri Kuu na Mapendekezo ya ajenda za Mkutano Mkuu;

(xix). Kuandaa hoja za kupelekwa Bungeni au Baraza la Wawakilishi na Wabunge au Wajumbe wa Baraza la Wawakillishi wa Chama;

(xx). Kuratibu utendaji wa ofisi ndogo ya Makao Makuu Zanzibar;

(xxi). Kusimamia utendaji kazi wa Ngome za Vijana, Wanawake na Wazee; na

(xxii). Endapo hatua zilizoainishwa katika ibara ndogo za (ix) na (x) za ibara hii zitachukuliwa, Kamati Kuu Taifa itawajibika kuweka Kaimu wa Kiongozi aliyesimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa, na pia kuweka uongozi wa muda kuchukua nafasi ya uongozi uliosimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii ila ijuilikane tu kiongozi yeyote anae Kaimu nafasi hiyo atakaimu kwa muda ulioelezwa na kwa utaratibu uliowekwa na Katiba hii.

(2) Kamati Kuu itaandaa rasimu ya bajeti ya kila mwaka ya mipango ya maendeleo ya Chama na fedha za matumizi kwa chama na kujadiliwa na baadae kupelekwa Halmashauri Kuu kuidhinishwa.

*Kamati ya Uongozi Taifa*

79A. (1) Kutakuwa na Kamati ya Uongozi Taifa ambayo wajumbe wake na kukutana kwake itakuwa kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 82(1) na (2) ya Katiba hii.

*Kazi za Kamati ya Uongozi ya Taifa*

(2) Kamati ya Uongozi ya Taifa itakuwa na majukumu yafuatayo: -

a. Kujadili jambo la dharura litakalotokea ambalo linahitaji uamuzi wa haraka na kisha kutoa maelekezo kwa vyombo vya utekelezaji;

b. Kutoa uongozi kwa mambo yote ya kitaifa ambayo hayakuelezwa wazi wazi ndani ya Katiba na kwamba utekelezaji wake hautokwenda kinyume na Katiba ya Chama, Katiba ya Nchi au Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria nyingine yoyote halali iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi.

c. Kufanya usuluhishi wa migogoro ya kiutendaji baina ya viongozi wakuu na wa Kitaifa wa Chama.

*Sekretarieti ya Kamati Kuu*

80. (1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Kamati Kuu Taifa ambayo itakutana mara moja kwa kila mwezi na inaweza kuitishwa kwa dharura wakati wowote Mwenyekiti wake atakapoona haja na umuhimu huo.

*Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati Kuu*

(2) Sekretarieti ya Kamati Kuu itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Katibu Mkuu.
(b) Manaibu Katibu Mkuu.
(c) Makatibu wa Idara za Chama Taifa.
(d) Manaibu Katibu wa Idara za Chama Taifa.
(e) Makatibu wa Ngome za Wanawake, Vijana na Wazee.

(3) Wajibu wa Sekretarieti ya Kamati Kuu utakuwa kama ifuatavyo:-

*Kazi na Wajibu wa Sekretarieti ya Kamati Kuu*

(a). Kuhakikisha kuwa Chama wakati wote kinakwenda na wakati katika mahusiano, mawasiliano na utendaji wa shughuli za Chama kisayansi na uyakinifu.
(b). Kutekeleza maagizo yote ya Mkutano Mkuu wa Taifa na Halmashauri Kuu ya Taifa.
(c). Kutekeleza kazi za kila siku za Chama ngazi ya Taifa.
(d). Kutunza, kuhifadhi na kulinda mali, vyombo, nyaraka na vitendea kazi mbalimbali vya Chama katika ngazi ya Taifa.
(e). Kuandaa ajenda za Kamati Kuu, na mapendekezo ya ajenda za Halmashauri Kuu ya Taifa na kutayarisha na

kuhifadhi mihtasari ya vikao vyote vya Mkutano Mkuu wa Taifa, Halmashauri Kuu ya Taifa na vya Kamati Kuu ya Taifa yenyewe, na kuwasilisha taarifa ya yatokanayo kutokana na utekelezaji wa maamuzi ya kikao kilichopita.

(f). Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Chama na kufikisha taarifa zake katika kila kikao cha Kamati Kuu ya Taifa.

(g). Kuandaa na kuendesha mafunzo ya siasa, uongozi na utendaji kwa viongozi na watendaji wa Chama kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya vyama vya siasa.

(h). Kupokea na kuchambua mapendekezo ya vikao vya chini na kuyafanyia kazi ipasavyo na pia kufikisha kwa vikao vya chini maamuzi na maelekezo ya vikao vya Taifa.

(i). Kuwateua na kuwapangia kazi watendaji na watumishi wa Chama wa Makao Makuu, Ofisi Kuu na Ofisi nyingine zilizoanzishwa na Kamati Kuu.

*Kamati za Mashauriano*

81. (1) Sekretarieti ya Kamati Kuu inaweza, ikiona inafaa kujigawa kwa Wajumbe waliyoko Tanzania Bara na kuwa Kamati ya Mashauriano kwa Tanzania Bara na wale waliyoko Zanzibar kuwa Kamati ya Mashauriano kwa Zanzibar.

(2) Kazi ya Kamati hizi za Mashauriano itakuwa ni kushauriana kuhusu mambo mbali mbali ya utendaji wa Chama lakini havitokuwa vikao vya maamuzi isipokuwa tu pale inapotokea haja na ulazima kutokana na dharura inayokuwa imejitokeza na kwamba kusubiri kwake vikao vya kawaida vya Chama vinaweza kuathiri taswira, uhai na/au ustawi wa Chama kwa sharti kuwa maamuzi hayo baadaye yatapelekwa katika vikao vya juu ili kuthibitishwa.

## SEHEMU YA NANE

## VIONGOZI WAKUU

*Viongozi Wakuu wa Chama*

82. (1) Kutakuwa na Viongozi Wakuu wa Chama wafuatao:-

(i). Kiongozi wa Chama;
(ii). Mwenyekiti wa Chama;
(iii). Makamu wa Mwenyekiti;
(iv). Katibu Mkuu wa Chama;
(v). Manaibu Katibu Mkuu;
(vi). Mwanasheria Mkuu wa Chama; na
(vii). Mshauri Mkuu wa Chama;

(2) Viongozi wote waliotajwa katika Ibara ya 82(1) wataunda Kamati ya Uongozi ambayo Mwenyekiti wake atakuwa ni Kiongozi wa Chama na watakutana mara kwa mara pale Mwenyekiti wa kikao atapokiitisha.

(3) Kwa kuleta uwiano mzuri wa Chama Kitaifa, ikiwa Mwenyekiti wa Chama amechaguliwa kutoka upande mmoja wa Muungano, basi Katibu Mkuu atatoka upande wa pili wa Muungano.

(4) Kutakuwa na Makamu wawili wa Mwenyekiti Taifa, mmoja atachaguliwa kutoka Tanzania Bara na wa pili kutoka Zanzibar ambao wote watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(5) Manaibu Katibu Mkuu wa Chama watakuwa wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na wapili kutoka Zanzibar ambao watateuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti kwa kushauriana na Makamu wote wa Mwenyekiti.

*Kiongozi wa Chama na Majukumu yake*

83. (1) Kutakuwa na Kiongozi wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Atakuwa kiongozi wa Chama na Mwenyekiti wa Kikao cha Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia;
(b) Atakuwa mkuu wa siasa, mshauri na mwelekezaji mkuu kwa viongozi wote na maafisa wa Chama.
(c) Atateua wajumbe watano wa Kamati Kuu baada ya

kushauriana na Mwenyekiti wa Chama Taifa na kuthibitishwa na Halmashauri Kuu kwa mujibu wa Katiba hii;

(d) Atapendekeza majina ya Washauri wa Chama;

(e) Atakuwa mtoa tamko rasmi kuhusu masuala ya sera na mtazamo wa Chama katika mambo ya kitaifa na kimataifa;

(f) Atakuwa mtoa habari mahsusi kwenye Mkutano Mkuu, Halmashauri Kuu na Kamati Kuu kuhusu hali ya kisiasa nchini na masuala mengine ya kitaifa na kimataifa;

(2) Iwapo kiti cha Kiongozi wa Chama kitakuwa wazi kwa sababu ya kujiuzulu, kuondoka katika chama, kuvuliwa uongozi au uanachama, maradhi yenye kuondoa uwezo wa kufanya kazi au kifo, Mkutano Mkuu Maalum wa Taifa utaitishwa katika muda usiozidi miezi kumi na miwili tangu kuwa wazi kwa kiti hicho kwa ajili ya kuchagua Kiongozi wa Chama mwingine, au ikiwa Mkutano Mkuu wa Taifa utafanywa mbele yake, na si muda mrefu, basi pale utakapofanyika Mkutano Mkuu huo kwa ajili ya kuchagua kiongozi wa Chama mwengine.

Isipokuwa tu iwapo kutokuwepo kwa Kiongozi wa Chama hakutokani na sababu zilizotajwa hapa, basi Kiongozi wa Chama baada ya kushauriana na Mwenyekiti, atamkabidhi miongoni mwa wajumbe wa Kamati Kuu kutekeleza majukumu ya Kiongozi wa Chama kwa kadri yatakavyoainishwa kwenye Hati ya makabidhiano katika kipindi hicho ambacho Kiongozi wa Chama hayupo.

*Mwenyekiti wa chama Taifa*

84. (1). Kutakuwa na Mwenyekiti Chama Taifa ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(2) Mwenyekiti wa Taifa atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Atakuwa mlinzi mkuu wa sera zilizopendekezwa na kupitishwa au jambo lolote litakaloamuliwa na kupitishwa na vikao vya chama;

(ii) Atahakikisha kuwa ngazi zote za chama zinatekeleza maamuzi yaliyotolewa na vikao;

(iii) Atahakikisha kuwa ngazi zote zinafanya kazi ndani ya mipaka ya Katiba, Kanuni, sera na maamuzi

yoyote yaliyoagizwa na vikao vikuu vya chama;

(iv) Atafuatilia na kuratibu masuala ya amani, utulivu na nidhamu katika Chama;

(v) Atakuwa mwenyekiti wa mikutano yote ya chama ya kitaifa isipokuwa Mkutano Mkuu wa Kidemokrasia;

(vi) Atafanya shughuli nyingine za Chama kama atakavyoelekezwa na vikao vya Chama na vikao vya Utendaji;

(vii) Katika mikutano anayoiongoza pamoja na kuwa na kura yake ya kawaida atakuwa pia na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafika zitalingana.

(3) Iwapo Mwenyekiti wa Chama hayupo kwa sababu yoyote ile basi Makamu Mwenyekiti ambaye anatoka upande mwengine wa Muungano tofauti na anaotoka Mwenyekiti, na kama Makamu Mwenyekiti aliyetajwa kwanza naye hayupo, basi Makamu Mwenyekiti aliyebakia atakaimu nafasi ya uenyekiti.

(4) Iwapo kiti cha Mwenyekiti wa Chama kitakuwa wazi kwa sababu ya kujiuzulu, kuondoka katika Chama, kuvuliwa uongozi au uanachama, maradhi yenye kuondoa uwezo wa kufanya kazi au kifo, Mkutano Mkuu maalumu wa Taifa utaitishwa katika muda usiozidi miezi kumi na mbili tangu kuwa wazi kwa kiti hicho ili kuchagua Mwenyekiti mwingine. Katika muda huo, Makamu Mwenyekiti ambaye anatoka upande mwengine wa Muungano atakaimu nafasi hiyo hadi pale Mwenyekiti mpya atakapochaguliwa.

(5) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kumsimamisha Mwenyekiti wa Chama kwa kupiga kura ya kutokuwa na imani naye kwa maamuzi ya zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa. Hata hivyo, kura ya kutokuwa na imani haitapigwa hadi kuwe na hoja maalumu kwa ajili hiyo na ambayo imeungwa mkono na theluthi mbili ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wajumbe kutoka Zanzibar.

(6) Mwenyekiti wa Chama ataweza kuondolewa kwenye madaraka baada ya mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya

Taifa kwa azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa litakaloungwa mkono na idadi ya nusu ya kura za wajumbe halali waliohudhuria na kupiga kura.

*Mshauri Mkuu wa Chama*

85. (1) Kutakuwa na Mshauri Mkuu wa Chama ambaye atateuliwa na Kiongozi wa Chama baada ya kumpendekeza jina lake kwa Halmashauri Kuu ya Chama na kukubaliwa.

(2) Mshauri Mkuu wa Chama atakuwa ni mtu mwenye busara, fikra nzuri, maadili, mpenda amani, mpigania haki na kwamba amekuwa katika siasa za Nchi au za Kimataifa kwa kipindi kirefu sana.

(3) Kazi na wajibu wa Mshauri Mkuu wa Chama ni: -

(i) Kukishauri Chama juu ya namna ya kukiimarisha;
(ii) Kumshauri Kiongozi wa Chama;
(iii) Atawatembelea Wanachama popote walipo kwa ajili ya kuwahamasisha na kuwapa ari na morari ya kukiimarisha Chama.
(iv) Atafanya shughuli nyingine yoyote atakayoombwa na Chama kuifanya, au shughuli nyingine yoyote ambayo kwa hekima zake anahisi ni kwa faida na maslahi ya Chama na Wanachama.

(4) Kiongozi wa Chama anaweza kuteuwa washauri wengine wa Chama wasiozidi watatu miongoni mwao angalau mmoja wao awe ni mwanamke na ambao atawaelekeza kazi wanazotakiwa kuzifanya pamoja na masharti na utaratibu wa kuzifanya kazi hizo.

*Makamu Mwenyekiti Taifa na kazi zake*

86. (1) Kutakuwa na Makamu wawili wa Mwenyekiti, mmoja kutoka Tanzania Bara na wa pili kutoka Zanzibar ambao watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

(2) Pale ambapo Mwenyekiti anatokea upande mmoja wa Muungano, basi Makamu wa Mwenyekiti anaetokea upande wa pili wa Muungano ndiye atakayemtangulia mwenzake katika shughuli za Kichama na Kitaifa.

(3) Majukumu ya Makamu Mwenyekiti yatakuwa ni:-

(a) Wasaidizi wakuu wa Mwenyekiti wa Chama na watafanya kazi zozote za Chama watakazopewa na Mwenyekiti wa Chama Taifa;

(b) Watakuwa washauri wa chama katika maeneo yao (Bara na Zanzibar) na wote watakuwa na hadhi sawa sawa ila pale ambapo Katiba imeeleza vinginevyo;

(c) Makamu Mwenyekiti Zanzibar ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati Maalumu ya Zanzibar na yule wa Tanzania Bara atakuwa Mwenyekiti wa Kamati Maalumu ya Tanzania Bara;

(d) Watamshauri Mwenyekiti katika majukumu yake ya kila siku kwa maeneo yao;

(e) Watakuwa Walezi wa Ngome za Chama;

(f) Watakuwa wahamasishaji wa chama katika maeneo yao; na

(g) Watakaimu nafasi ya Mwenyekiti kama hayupo kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Katiba hii;

(h) Halmashauri Kuu inaweza kumsimamisha Makamu Mwenyekiti kwa kupiga kura ya kutokuwa na imani naye na ambayo itaungwa mkono na zaidi ya nusu ya wajumbe wote waliohudhuria kikao wakati hoja hiyo inatolewa.

*Katibu Mkuu*

87. (1) Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Chama ambaye atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Ibara ya 76(1)(c) ya Katiba hii. .

*Kazi na Wajibu wa Katibu Mkuu*

(2) Kazi na wajibu wa Katibu Mkuu wa Chama itakuwa kama ifuatavyo: -

(i) Atakuwa Katibu wa mikutano ya chama katika ngazi ya Taifa;

(ii) Atakuwa ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za utendaji za Chama;

(iii) Ataitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Kamati Kuu ya Chama kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa ajenda za Kamati Kuu na

kuchukua hatua za utendaji wa maamuzi ya Chama;

(iv) Atakuwa na uwezo wa kuajiri, kuachisha kazi na kusimamia nidhamu ya watumishi wote wa Chama kwa kushauriana na sekretarieti ya Chama kwa mujibu wa Katiba, Kanuni, taratibu za Chama na sheria za nchi;

(v) Atakuwa na wajibu wa kuandaa na kuitisha mikutano yote ya vikao vya Chama katika ngazi ya Taifa kwa kushauriana na Kiongozi wa Chama na Mwenyekiti wa Chama, na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya Chama;

(vi) Atakuwa muwajibikaji Mkuu wa mambo yote ya fedha na pia mdhibiti mkuu wa mali za Chama zinazohamishika na zisizohamishika;

(vii) Atajenga mahusiano mema na makatibu wakuu wa vyama vyingine vya siasa ndani ya nchi;

(viii) Atakuwa na dhamana ya Ofisi za Makao Makuu, Ofisi Kuu, Ofisi ndogo za Makao Makuu na Ofisi za Kanda za Chama;

(ix) Atahakikisha kwamba nyaraka zote za Chama pamoja na kumbukumbu za vikao vyote vya Chama vya Taifa zinatunzwa na kuhifadhiwa vizuri;

(x) Atafanya kazi nyingine yoyote itakayokuwa imetajwa penginepo katika Katiba hii na/au kwa maelekezo ya vikao vya Chama au viongozi wa juu yake;

(xi) Halmashauri Kuu itakuwa na uwezo wa kumuondoa Katibu Mkuu kwa kupiga kura ya kutokuwa na imani na kama kura hiyo itaungwa mkono na zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria.

*Manaibu Katibu Mkuu*

88. (1) Kutakuwa na Manaibu Katibu Mkuu wawili, mmoja akitokea upande mmoja wa Muungano na wa pili upande wa pili wa Muungano.

(2) Naibu Katibu Mkuu ambaye atatoka upande ambao hatoki Katibu Mkuu, ndiye atakuwa anamtangulia mwenzake.

(3) Manaibu Katibu Mkuu hawa watakuwa na mamlaka sawa kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano na watachaguliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa baada ya Mwenyekiti wa Chama kushauriana na Makamu Mwenyekiti na Kiongozi wa Chama na kupendekeza majina mawili kwa Halmashauri Kuu kwa ajili ya kupigiwa kura.

(4) Kazi na wajibu wa Naibu Katibu Mkuu ni pamoja na:-

(i) Kuandaa na kuitisha mikutano ya Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya Chama Taifa na vikao vya Mashauriano kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

(ii) Manaibu Katibu Mkuu wa Chama watakuwa ndio wasaidizi wakuu wa Katibu Mkuu wa Chama na watafanya kazi zozote za Chama watakazopewa na Katibu Mkuu wa Chama au Kiongozi wa Chama au Mwenyekiti wa Chama Taifa;

(iii) Watakuwa Makatibu wasaidizi wa vikao vyote vya Chama wakimsaidia Katibu Mkuu;

(iv) Watamsaidia Katibu Mkuu kusimamia shughuli, taratibu na Kanuni zote za Kiutawala za Chama za kila siku;

(v) Watakuwa wajumbe wa vikao vyote ambavyo Katibu Mkuu wa Chama Taifa anashiriki kwa wadhifa wake;

(vi) Watafanya kazi nyingine zozote za Chama zitakazokuwa zimetajwa penginepo katika Katiba hii na/au kwa maelekezo ya Vikao vya Chama au viongozi wa juu yao.

(5) Iwapo Katibu Mkuu ni mgonjwa au hayupo nchini au ana sababu nyingine ambazo zinamfanya asihudhurie kikao,

basi shughuli zake zitakaimiwa na Naibu Katibu Mkuu ambaye hatoki upande wa Muungano anaotoka Katibu Mkuu.

*Mwanasheria Mkuu wa Chama*

89. (1) Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Chama atakaeteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Uongozi wa Chama;

(2) Mwanasheria Mkuu wa Chama atakuwa ni Mwanachama mwenye sifa za kuwa Wakili katika Upande wowote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na awe na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka mitano.

(3) Mwanasheria Mkuu wa Chama atakuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa kutokana na wadhifa wake na anaweza kuhudhuria vikao vyote vya Sekretarieti ya Chama ikiwa ataalikwa kutoa ushauri wa kisheria kwa jambo lolote mahsusi ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo.

(4) Kazi na wajibu wa Mwanasheria Mkuu wa Chama ni pamoja:-

(i) Atakuwa Mshauri Mkuu wa kisheria kwa Chama, na atatekeleza shughuli zote za kisheria zitakazopelekwa kwake au atazaoagizwa na Mwenyekiti au kwa Mujibu wa Katiba hii au miongozo mingine ya Chama;

(ii) Atakiwakilisha Chama kwenye mashauri yote ya Madai na ya Kikatiba ambayo Chama kitayafungua au kufunguliwa kwenye Mahakama yoyote ya Tanzania na Nje ya Tanzania;

(iii) Kushiriki na kutoa maoni kwenye majadiliano ya mkataba ambao Chama kinakusudia kuingia na Mtu au Taasisi yoyote;

(iv) Kutoa maoni kwa kambi za wabunge na wawakilishi wanaotokana na ACT Wazalendo juu ya miswada ya sheria inayowasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi au Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(v) Mwanasheria Mkuu wa Chama atakuwa na wajibu wa kulinda na kuhakikisha uwepo wa uongozi unaofuata na kuheshimu sheria ndani na Nje ya Chama na kulinda maslahi ya Umma.

(4) Majukumu na wajibu wa Mwanasheria Mkuu wa Chama yaliyotajwa katika Ibara ndogo ya (3) ya Ibara hii, yanaweza

kutekelezwa na yeye mwenyewe au kukasimiwa kwa mwanachama mwengine yeyote alie na uzoefu wa mambo ya sheria, mradi tu kuwe na maelekezo ya utekelezaji wa kazi hiyo.

## SURA YA NNE

## KAMATI MAALUM ZA KAMATI KUU KAMATI ZA MAADILI, TAASISI, IDARA ZA CHAMA, MAKOSA, NIDHAM NA UTATUZI WA MIGOGORO

## SEHEMU YA KWANZA

## KAMATI MAALUM ZA KAMATI KUU

*Kamati Maalum za Kamati Kuu*

90. (1) Kutakuwa na Kamati maalum mbili za Kamati Kuu, moja kwa upande wa Tanzania Bara na ya pili kwa Zanzibar.

(2) Kazi za Kamati hizo zitakuwa sawa sawa, isipokuwa kila moja itashughulikia eneo lake la utendaji ambalo ni Tanzania Bara kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili.

(3) Kamati Maalumu za Kamati Kuu zitafanya vikao vyake wiki moja kabla ya tarehe iliyopangwa kufanyika kwa kikao cha Kamati Kuu ya Chama Taifa au muda wowote ule kwa dharura ikiwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Kamati Kuu ataona kuna haja ya kufanya hivyo.

*Kazi na wajibu wa Kamati Maalum*

91. Kazi na wajibu wa Kamati maalum zitakuwa kama ifuatavyo:-

a. Kutoa mapendekezo kwa Kamati Kuu juu ya masuala mbalimbali yahusuyo Tanzania Bara kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili;
b. Kusimamia utendaji wa Sekretarieti ya ofisi ya Makao Makuu Tanzania Bara kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili;
c. Kupendekeza utekelezaji wa mambo ya kisera yahusuyo Tanzania Bara kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili;
d. Kuleta mapendekezo kwa Kamati Kuu juu ya uteuzi wa wagombea ubunge na uwakilishi na wale wa Viti Maalum kwa upande wa Tanzania Bara kwa upande mmoja na kwa Zanzibar kwa upande wa pili kabla ya Kamati Kuu kufanya uteuzi wa mwisho;
e. Kuteua maafisa wa idara mbalimbali za Ofisi Kuu ya Makao

Makuu kwa upande wa Zanzibar na vile maafisa wa idara hizo kwa Makao Makuu, Dar esalam;

f. Kuratibu shughuli za chama Tanzania Bara kwa upande mmoja na kwa Zanzibar kwa upande wa pili;
g. Kutoa ushauri na misaada ya kiutendaji kwa uongozi wa ACT katika Mikoa ya Tanzania Bara kwa upande mmoja na kwa Mikoa ya Zanzibar kwa upande wa pili;
h. Kuratibu shughuli za kampeni za wagombea Urais wa Muungano na Urais wa Zanzibar katika eneo lote la Zanzibar kwa upande mmoja na shughuli kama hizo kwa Tanzania Bara kwa upande wa pili;
i. Kuratibu na kuunganisha shughuli za Ngome za Chama Zanzibar kwa upande mmoja na kwa Tanzania Bara kwa upande mwengine;
j. Kuwa kiunganishi cha Chama na shughuli za kiserikali;
k. Kuratibu na kutoa taarifa kwa Chama ngazi za juu kuhusu hali ya kisiasa, kijamii na kiutawala;
l. Kuandaa mikakati na kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Chama Zanzibar kwa upande mmoja na Tanzania Bara kwa upande wapili;
m. Kusimamia misingi mikuu ya Chama Zanzibar kwa upande mmoja na kwa Tanzania Bara kwa upande mwengine;
n. Kuhakikisha chama kinaenea Tanzania Bara yote kwa upande mmoja na Zanzibar yote kwa upande wa pili;
o. Kufanya uteuzi wa awali wa mgombea Uspika na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;
p. Kupendekeza kwa Kamati Kuu maoni ya mambo ambayo wanahisi kuwa kuna haja na ulazima wa kurekebisha na au kusahihisha ibara au baadhi ya ibara za Katiba ya chama kwa sharti kuwa Kamati Kuu kwa busara zake inaweza kuyakubali maoni hayo na:
    i. Kuyapeleka Halmashauri Kuu kwa kujadiliwa ili nayo ikiwa yamekubaliwa yapelekwe katika kikao cha Mkutano Mkuu kwa kuzingatiwa na kupitishwa, au
    ii. Kuyarudisha maoni hayo pamoja na maagizo ya kupelekwa katika ngazi za chini za chama kupata maoni yao.

*Wajumbe wa Kamati Maalum*

92. (1) Kwa upande wa Tanzania Bara, Wajumbe wa Kamati Maalumu watakuwa ni:-
    (a) Makamu Mwenyekiti kutoka Tanzania Bara.
    (b) Katibu Mkuu ikiwa atatokea Tanzania Bara
    (c) Naibu Katibu Mkuu Bara
    (d) Wajumbe wote wa Kamati Kuu wanaotoka Tanzania Bara.

(2) Kwa upande wa Zanzibar Wajumbe wa Kamati Maalum watakuwa, kwa mpangilio huo huo wa Tanzania Bara kama ilivyoelezwa chini ya Ibara 92(1).

**SEHEMU YA PILI**

**IDARA NA NGOME ZA CHAMA**

*Halmashauri Kuu kuanzisha Idara*

93. (1) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kuanzisha Idara ya aina yoyote ile katika ngazi ya Taifa ili kusaidia utekelezaji mzuri wa shughuli za Chama.

(2) Kila Idara ya Chama na Ngome za Chama ngazi ya Taifa itaongozwa na Katibu akisaidiwa na Naibu Katibu atakayetoka upande tofauti wa Jamhuri ya Muungano ambao Katibu wake anatoka.

(3) Kamati za Uongozi za Ngome Taifa na Kamati za Uongozi za Ngome na Chama katika ngazi ya Mkoa, Jimbo, Kata na/au Tawi zinaweza kuanzisha Idara za aina yoyote ile katika ngazi husika ili kusaidia utekelezaji mzuri wa shughuli za Chama.

(4) Katibu Mkuu kwa kushauriana na Kiongozi wa Chama, Mwenyekiti Taifa na Makamu Wenyeviti ndiye atakayependekeza Makatibu na Manaibu Katibu wa Idara ambao watathibitishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(5) Makatibu wa Ngome na Makatibu wa Chama ngazi za Mikoa, Jimbo, Kata na Tawi kwa kushauriana na Wenyeviti wa ngazi

husika watapendekeza majina ya Makatibu na Manaibu Katibu wa Idara na kuyawasilisha kwenye Kamati za Uongozi kwa uteuzi.

(6) Majukumu ya kila Katibu na Naibu Katibu wa Idara wa kila ngazi zitaelezewa mara kwa mara katika Kanuni za Uendeshaji Chama na Miongozo ya Ngome.

*Ngome za Chama*

94. (1) Kutakuwa na Ngome za Chama zitakazofanya shughuli zake kwa mujibu wa Miongozo ya ngome husika itakayotungwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa.

(2) Ngome za Chama zilizoanzishwa chini ya Katiba hii ni:-

(a) Ngome ya Wanawake
(b) Ngome ya Vijana na
(c) Ngome ya Wazee

(3) Kila ngome itakuwa na:-

(i) Mwenyekiti wa Ngome atakayekuwa Kiongozi Mkuu na msemaji Mkuu wa Ngome na atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa wa Ngome husika.

(ii) Makamu Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa wa Ngome husika kwa masharti kwamba ikiwa Mwenyekiti ametoka upande mmoja wa Muungano basi Makamu Mwenyekiti atatoka upande mwingine wa Muungano.

(iii) Katibu na Naibu Katibu ambao watateuliwa na Halmashauri Kuu kwa utaratibu ule ule wa Katibu Kutoka upande mmoja wa Muungano na Naibu wake kutoka upande mwengine wa Muungano.

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza ikiona inafaa na ni kwa maslahi ya Chama, kuelekeza, kuthibitisha na/au kubatilisha maamuzi yoyote yaliyofanywa na Ngome katika ngazi

yoyote ile.

(5) Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Ngome na bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, kila Ngome katika ngazi husika itawajibika kwa Chama katika ngazi hiyo.

## SEHEMU YA TATU
## BODI YA WADHAMINI, KAMATI NA TAASISI NYENGINE
## BODI YA WADHAMINI

*Bodi ya Wadhamini*

95. (1) Kutakuwa na Bodi ya wadhamini ya Chama itakayoteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kwa mujibu wa Sheria za Nchi kwa kipindi cha miaka mitano (5) na mjumbe anaweza kuteuliwa tena baada ya muda wake kumalizika.

(2) Bodi itakuwa na Wajumbe wasiozidi Tisa (9), watano (5) kutoka Tanzania Bara na angalau mmoja (1) ni mwanamke na wanne (4) kutoka Zanzibar angalau mmoja (1) ni mwanamke ambao watateuliwa kwa masharti yanayohitajika na Sheria ya Bodi ya Wadhamini na utaratibu uliowekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(3) Bodi ya Wadhamini itakuwa ndiyo mdhamini pekee wa fedha na mali za Chama zote zinazohamishika na zisizo hamishika pamoja na madeni na itafanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na sheria za nchi zinazohusu Wadhamini.

(4) Bodi inaweza kushitaki au kushitakiwa kwa niaba ya chama.

(5) Bodi itawajibika kwa Halmashauri Kuu ya Taifa ambayo itaweka utaratibu unaofaa wa kuendesha shughuli za Bodi, na itafanya vikao vyake angalau mara tatu kwa mwaka.

(6) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini watachaguliwa na Wajumbe wa Bodi kutoka miongoni

mwao, kwa sharti kwamba Mwenyekiti akitoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti atatoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

(7) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi watakuwa ni Wajumbe wa Kamati Kuu.

(8) Katibu anaeshughulikia masuala ya fedha na uchumi katika Chama, kwa nafasi yake, atakuwa Katibu wa Bodi ya Wadhamini.

(9) Mdhamini anaweza kuondolewa na Halmashauri Kuu ya Taifa ikiwa atafanya kosa lolote lile ambalo Kiongozi yeyote wa Chama akilifanya chini ya Katiba hii anaweza kuondolewa.

(10) Bodi ya Wadhamini itawajibika kutoa taarifa ya utendaji wake ya kila miezi sita kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

*Kamati na Taasisi nyingine*

96. (1) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza, ikiona inafaa na ni kwa maslahi ya Chama, kuanzisha Kamati, Tume au Taasisi yoyote ile ya Kitaifa yenye lengo la kusaidia utekelezaji mzuri wa sera na itikadi za Chama au kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote lile linalohitajiwa kufanyiwa uchunguzi.

(2) Pale ambapo Halmashauri Kuu ya Taifa imeanzisha Kamati au Taasisi au Tume yoyote ya Kitaifa kwa ajili ya jambo fulani, pia itatoa maelekezo ya namna:-

(a) Wajumbe wake watakavyopatikana;
(b) Hadidu za rejea za chombo hicho;
(c) Muda wa kufanya kazi hiyo;
(d) Jambo jingine lolote ambalo Halmashauri Kuu inaweza kuelekeza.

## SEHEMU YA NNE

## KAMATI ZA MAADILI

*Kuanzishwa kwa*

97. (1) Kutakuwa na Kamati za maadili katika ngazi zifuatazo za Chama:-

*Kamati za Maadili*

(i) Tawi;
(ii) Kata;
(ii) Jimbo;
(iii) Mkoa; na
(iv) Taifa.

(2) Kamati za maadili za Tawi, Kata, Jimbo na Mkoa zitateuliwa kwa mpangilio na Mwenyekiti wa Tawi, Kata, Jimbo au Mkoa baada ya kuidhinishwa kwao na Kamati ya Uongozi inayohusika na zitakua na Wajumbe wasiozidi watano (5) miongoni mwao wakiwemo wanawake angalau wawili (2) kwa kila Kamati.

(3) Kazi na majukumu ya Kamati za maadili za Kata, Jimbo na Mkoa zitakuwa zifuatazo:-

(i) Kufanya uchunguzi kamili, kwa uadilifu na weledi na bila upendeleo, kuhusu tuhuma zilizowasilishwa dhidi ya mwanachama, mjumbe, afisa, mwakilishi au kiongozi wa Chama katika ngazi husika;
(ii) Kutoa taarifa kwa maandishi kuhusu matokeo ya uchunguzi na sababu na mazingira yaliyosababisha kufikia hitimisho;
(iii) Kutoa adhabu yoyote kwa mujibu wa Katiba hii isipokuwa kusimamisha au kufukuza uanachama au uongozi;
(iv) Kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Uongozi ya ngazi yake kwa adhabu ambazo haina mamlaka nazo;

*Rufaa*

98. Mwanachama yeyote aliechukuliwa hatua za kinidhamu chini ya utaratibu uliowekwa katika sehemu hii, ikiwa anaona hakutendewa haki anaweza kukata rufaa ndani ya siku kumi na nne (14) kwa Kamati ya Maadili iliyopo ngazi ya juu, na maamuzi ya rufaa hiyo nayo yatolewe ndani ya wiki mbili kuanzia siku ilipopokelewa rufaa hiyo.

*Kamati ya Maadili ya Taifa*

99. (1) Kutakuwa na Kamati ya Maadili ya Taifa itakayokuwa na mamlaka ya kinidhamu kuhusu maafisa na viongozi katika

ngazi ya Taifa pamoja na viongozi na wanachama wengine waandamizi wakiwemo wabunge, wawakilishi, wajumbe wa Kamati Kuu Taifa, Wajumbe wa Halmashauri Kuu pamoja na masuala yote ya kinidhamu yatakayopelekwa mbele yake kutokana na vikao vya Kamati Kuu au Halmashauri Kuu.

(2) Kamati ya Maadili itakuwa ni moja kati ya Idara huru za Chama.

(3) Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili atateuliwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa baada ya Mwenyekiti wa Taifa kwa kushauriana na Kiongozi wa Chama, Makamu Wenyeviti wote wawili kuwasilisha mapendekezo yake mbele ya Halmashauri Kuu kwa kuidhinishwa.

(4) Kutakuwa na Wajumbe wengine watano na wasiozidi tisa, kati yao wawili wakiwa wanawake watakaoteuliwa na Halmashauri Kuu kwa utaratibu ule ule alioteuliwa Mwenyekiti wa Kamati.

(5) Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili atakuwa mwanachama wa ACT ambaye angalau ana shahada ya Sheria au Shahada nyingine yoyote ya Chuo Kikuu kinachotambuliwa na mamlaka husika nchini, mwaminifu, mwenye uelewa wa Chama na siasa za nchi na dunia.

(6) Kwa wadhifa wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili Taifa atakuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Taifa na atatakiwa kutoa ripoti yake mara kwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(7) Katibu na Naibu Katibu wa Kamati ya Maadili watateuliwa na Halmashauri Kuu na kazi zake zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika barua yake ya uteuzi.

(8) Muda wa Wajumbe wa Kamati hii ni miaka mitano kuanzia siku waliyoteuliwa isipokuwa Halmashauri Kuu ya Taifa

inaweza, ikiona inafaa, yaweza kuwateuwa tena Wajumbe wa Kamati baada ya muda wao kumalizika.

*Majukumu ya Kamati ya Maadili Taifa*

100. (1). Majukumu ya Kamati ya Maadili ya Taifa yatakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatilia nyendo za wanachama na viongozi wa Chama ili kuhakikisha kuwa kila mmoja miongoni mwao anatunza maadili mema ya Chama na maadili ya Uongozi;

(b) Kuhakikisha kuwa wanachama na Viongozi wanakuwa na nidhamu ndani ya Chama na nje ya Chama ili kukijengea taswira njema Chama katika umma;

(c) Kufanya uchunguzi juu ya taarifa za uvunjifu wa maadili na nidhamu zinazotolewa dhidi ya mwanachama, kiongozi, au kikao cha Chama, na kuchukua hatua kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au Kanuni zilizotungwa kwa ajili hiyo;

(d) Kufanya jambo jingine lolote ambalo Kamati itaagizwa na Halmashauri Kuu ya Taifa, lifanywe au ambalo Kamati yenyewe wataliona linafaa kufanywa kwa madhumuni ya kukilinda na kukinusuru Chama;

(2). Katika kutekeleza kazi na majukumu yake, Kamati ya Maadili wakati wowote itazingatia sheria za nchi kanuni, katiba hii ya Chama na kanuni zake pamoja na maamuzi ya haki za asili (natural justice) katika kufikia maamuzi yake.

(3). Kamati ya Maadili ya Taifa itakuwa ni msimamizi wa Kamati za Maadili za Mikoa, Majimbo, Kata na Tawi na itatoa maelekezo mara kwa mara pamoja na miongozo ya kazi zao ikiona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zao.

## SEHEMU YA TANO

## NIDHAMU, MAKOSA NA UTATUZI WA MIGOGORO KATIKA CHAMA

*Maamuzi ya Chama*

101. (1) Mapendekezo yoyote ya kuimarisha au kuendeleza Chama yanaweza kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu kwa kufanyiwa kazi na maamuzi yatatoka ngazi ya juu kwenda ngazi ya chini kwa utekelezaji.

(2) Katika ngazi moja yoyote ile, mapendekezo yatatoka katika kikao cha chini kwenda kikao cha juu kwa kufanyiwa kazi na maamuzi yatatoka kikao cha juu kwenda kikao cha chini kwa utekelezaji.

*Mapendekezo kutoka ngazi moja ya Chama*

102. (1) Bila ya kuathiri Ibara ya (1) ya ibara ya 101, mapendekezo yoyote ya kuimarisha Chama yanaweza pia yakatoka katika ngazi moja na kufanyiwa kazi na ngazi hiyo hiyo na kwamba inaweza pia kutoa uamuzi wake ambao unaweza kusahihishwa au kubatilishwa na ngazi yoyote iliyopo juu yake.

(2) Bila ya kuathiri Ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 101, mapendekezo yote ya kuimarisha chama yanaweza pia yakatoka katika kikao kimoja na kufanyiwa kazi na kikao hicho na kwamba kinaweza pia kutoa uamuzi wake ambao unaweza kusahihishwa au kubatilishwa na kikao chochote kilichopo juu yake.

(3) Maamuzi yoyote yanayotolewa na ngazi yoyote ile yatakuwa sahihi na halali hadi hapo maamuzi hayo yatakapobatilishwa au kutenguliwa na vikao halali vya ngazi iliyoko juu yake.

*Utatuzi wa Migogoro*

103. (1) Pale ambapo pametokea mgogoro wa aina yoyote ile:-

a) Baina ya mwanachama na mwanachama; au
b) Baina ya Tawi na Tawi au ngazi nyingine yoyote,

Na ikiwa Chama kinahisi ni vyema kwa mgogoro huo kusawazishwa kirafiki na kidugu bila ya kutumia Kamati za Maadili, basi Kamati Kuu ya

Taifa inaweza kuutatua mgogoro huo kwa njia ya usuluhisho baina ya pande hizo mbili kwa kuteua Kamati Maalum kwa ajili hiyo.

(2) Kamati Kuu inaweza kuweka utaratibu na mwongozo wa kuzingatia wakati wa uteuzi wa wajumbe wa Kamati hiyo ambapo haitozidi wajumbe watano angalau mmoja wao akiwa mwanamke.

(3) Mwanachama au Kiongozi yeyote yule anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu zifuatazo: -

(i) Karipio;
(ii) Karipio kali;
(iii) Onyo;
(iv) Onyo kali;
(v) Onyo la maandishi;
(vi) Kuachishwa nafasi ya uongozi aliyonayo katika Chama;
(vii) Kusimamishwa uanachama kwa kipindi kisichozidi miezi sita;
(viii) Kusimamishwa uanachama kwa kipindi kisichozidi miezi sita huku akiwa chini ya uangalizi maalumu;
(ix) Kusimamishwa kugombea nafasi yoyote ile katika Chama au nafasi ya serikali kwa tiketi ya Chama kwa kipindi kisichozidi miaka miwili;
(x) Kufukuzwa uanachama.

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa au Kamati Kuu au chombo kingine chochote kilicho na mamlaka ya kuchukua hatua za kinidhamu chini ya Katiba hii, kinaweza kuchukua hatua za kinidhamu kwa mpangilio ulioelezwa katika kifungu cha 103(3) cha Katiba hii, kuchukua hatua yoyote ile miongoni mwa hizo au zaidi, kutegemea uzito wa kosa alilotuhumiwa nalo mwanachama au kiongozi mradi tu chombo kinachochukua hatua hizo kiwe kimeridhika kwamba kosa hilo limetendeka.

(5) Maamuzi yoyote ya hatua za kinidhamu yaliyochukuliwa dhidi ya mwanachama au kiongozi wa Chama, yanaweza kukatiwa rufaa kwa ngazi ya rufaa iliyoko juu yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii ndani ya siku kumi na nne tangu siku uamuzi

ulipotolewa.

(6) Makosa yanayoweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ni pamoja na:-

(i) Kukiuka miiko na maadili ya uongozi kama yalivyoainishwa katika Kanuni za Mwenendo na Maadili ya Viongozi zitakazotungwa mara kwa mara na Kamati Kuu ya Taifa;
(ii) Kukataa kutekeleza wajibu au majukumu ya kikatiba;
(iii) Kufanya fujo au kutoa vitisho dhidi ya mwanachama au kiongozi mwingine;
(iv) Kughushi au kutoa taarifa za uongo kuhusu mahesabu au madai ya uongo kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia isiyo halali;
(v) Kuharibu mali ya Chama kwa makusudi;
(vi) Kupinga Itikadi, Falsafa, misingi, Katiba au sera za Chama katika majukwaa ya kisiasa;
(vii) Kusababisha mgawanyiko ndani ya Chama;
(viii) Kufanya kitendo chochote ambacho kinagharimu au kuharibu taswira ya Chama au taifa katika umma;

(7) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, viongozi watokanao na Chama ni:

(i) Naibu Katibu Mkuu
(ii) Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa
(iii) Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini
(iv) Waziri Mkuu atokanae na Chama
(v) Kiongozi wa upinzani Bungeni atokanae na Chama
(vi) Makamu wa Rais wa Zanzibar atokanae na Chama
(vii) Kiongozi wa upinzani katika Baraza la Wawakilishi atokanae na Chama
(viii) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano atokanae na Chama
(ix) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi atokanae na Chama
(x) Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wa Ngome
(xi) Katibu na Naibu Katibu wa Ngome
(xii) Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili
(xiii) Katibu na Naibu Katibu wa Kamati ya Maadili
(xiv) Kiongozi mwingine yeyote wa Chama na serikali wa

ngazi yoyote ile.

## SEHEMU YA SITA

## KUSITA KWA MWANACHAMA, KUJIUZULU UONGOZI NA KUFUKUZWA UANACHAMA

*Kuacha au Kuachishwa Uanachama*

104. (1) Mwanachama yeyote atasita kuwa mwanachama ikiwa:-

(a) Atajiuzulu mwenyewe;
(b) Atafukuzwa au kuachishwa uanachama na Tawi lake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii;
(c) Atafukuzwa au kuachishwa uanachama na Mkutano Mkuu wa Taifa au Kamati Kuu ya Taifa au Halmasharui Kuu ya Taifa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii;
(d) Atasita kulipa ada kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo;
(e) Atashindwa kuheshimu Katiba ya Chama au kuheshimu masharti ya uanachama;
(f) Atachukua uraia wa nchi nyingine;
(g) Atakuwa mwanachama wa chama kingine cha siasa;
(h) Atafariki dunia.

(2) Mtu yeyote aliyekoma uanachama chini ya Ibara ya 104(1) (b), (c), (d) au (e) ataweza kukata rufaa kwa ngazi ya juu yake, isipokuwa ijulikane tu kwa wale waliofukuzwa au waliothibitishwa kufukuzwa kwao na Mkutano Mkuu wa Taifa basi hakuna chombo chochote kingine katika Chama kitakachozungumzia uamuzi huo.

(3) Mtu yeyote anayepoteza uanachama wake chini ya Ibara ya 104 au ibara nyingine yoyote chini ya Katiba hii atapoteza haki zake zote za uanacahama na hatorudishiwa ada, zawadi, au ruzuku yoyote au kitu kingine chochote alichokitoa kwa Chama kabla ya kupoteza uanacahama wake.

(4) Uwezo wa kumuachisha uanachama mwanachama yeyote wa kawaida au kiongozi wa Chama wa Tawi uko mikononi mwa Tawi lake au Kamati Kuu ya Taifa au Halmashauri Kuu ya Taifa au Mkutano Mkuu wa Taifa.

(5) Mwanachama yeyote ambaye ana wadhifa katika Chama au Serikali (kiongozi kwa tiketi ya Chama) anaweza kuachishwa au kufukuzwa uanachama na Halmashauri Kuu ya Taifa au Mkutano Mkuu wa Taifa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(6) Mwanachama yeyote aliyesimamishwa uanachama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii hatoweza kugombea nafasi ya uongozi wowote ule wa Chama au serikali kupitia Chama mpaka ipite miezi sita tangu siku aliyosimamishwa.

(7) Mwanachama yeyote aliyejiuzulu au aliyeachishwa au aliyefukuzwa uanacahama anaweza kujiunga tena na Chama baada ya kupita miezi sita tangu aachishwe ikiwa atapeleka maombi yake kwa Tawi husika na kukubaliwa.

*Namna ya kujiuzulu*

105. (1) Mwanachama yeyote anaweza kutumia haki yake ya Kikatiba kwa kujiuzulu uanachama au uongozi katika Chama.

(2) Mwanachama atahesabiwa kuwa amejiuzulu na atakoma kuwa mwanachama:-

(a) Pindi anapotangaza hadharani uamuzi wake wa kutoendelea kuwa mwanachama na uanachama wake utakoma mara moja tangu siku alipotangaza; au

(b) Pindi akiandika barua kwa mamlaka ya Chama na barua hiyo kupokelewa.

*Kufukuzwa uanachama*

106. (1) Mwanachama yeyote anaweza kuachishwa au kufukuzwa uanachama ama na Tawi lake au na Kamati Kuu au Halmashauri Kuu ya Taifa au Mkutano Mkuu wa Taifa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa chini ya Katiba hii.

(2) Mwanachama yeyote ambae ana wadhifa katika Chama au serikalini kwa tiketi ya Chama hiki anaweza kuachishwa au kufukuzwa uanachama na Halmashauri Kuu ya Taifa au Mkutano Mkuu wa Taifa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(3) Mwanachama yeyote aliesimamishwa uanachama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii hatoweza kugombea nafasi ya uongozi wowote ule wa Chama au wa serikali kwa kupitia Chama, mpaka ipite miezi sita kuanzia siku

aliyosimamishwa.

(4) Mwanachama yeyote aliejiuzulu au aliyefukuzwa au aliyeachishwa uanachama anaweza kwa hiari yake na ikiwa bado anayakubali masharti ya uananchama, kujiunga tena na Chama hiki baada ya miezi sita tangu aachishwe au afukuzwe au alipojiuzulu uanachama.

(5) Mwanachama yeyote aliyepoteza uanachama wake kwa njia yeyote ile atapoteza haki zake zote za mwananchama na hatorudishiwa ada, zawadi, ruzuku au kitu kingine chochote alichokitoa kabla ya kupoteza uanachama isipokuwa ijuilikane tu kwamba ikiwa mwanachama huyo alikuwa na kitu chochote cha Chama, iwe mali, vifaa, chombo cha moto au cha aina nyingine yoyote basi atalazimika kuirejesha mali au chombo hicho kwa kwa Katibu wa ngazi aliopeleka barua yake ya kujiuzulu.

## SEHEMU YA SABA
## JUMUIYA ZA WABUNGE, WAWAKILISHI NA MADIWANI

*Jumuiya za Wabunge Wawakilishi na Madiwani*

107. (1) Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walioingia katika Bunge hilo kwa tiketi ya Chama hiki kwa pamoja wataunda jumuiya ya wabunge wa "ACT Wazalendo" katika Bunge hilo.

(2) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar walioingia katika Baraza la Wawakilishi kwa tiketi ya Chama hiki kwa pamoja wataunda jumuiya ya Wawakilishi wa "ACT Wazalendo" katika Baraza hilo.

(3) Madiwani wote waliochaguliwa kwa tiketi ya Chama wataunda jumuiya ya madiwani wa ''ACT Wazalendo".

(4) Jumuiya za Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wa ACT Wazalendo zinaweza kukutana mara kwa mara au inapotokea haja na umuhimu wa kufanya hivyo kwa minajili ya kujadili masuala muhimu ya Chama katika Kata, Majimbo na au Mikoa yao au kwa kujadili mambo mengine ambayo Chama kwa kupitia ngazi zake kitaelekeza.

*Kiongozi wa Wabunge,*

108. (1) Jumuiya ya Wabunge na/au ya Wawakilishi wa Chama itaongozwa na kiongozi atakayepatikana kwa mujibu wa

*Wawakilishi na Madiwani*

taratibu za Bunge na za Baraza la Wawakilishi na taratibu zilizowekwa na Kamati Kuu ya Taifa.

(2) Jumuiya ya Wabunge au ya Wawakilishi wa Chama inaweza kutunga Kanuni na taratibu zake ambazo Wabunge au Wawakilishi hao watahisi zinafaa kwa uendeshaji mzuri wa shughuli zao katika Bunge au katika Baraza la Wawakilishi, ila tu kanuni hizo ni lazima zithibitishwe na Katibu mwenye dhamana ya Bunge au Baraza la Wawakilishi kabla ya kuanza kutumika kwa kanuni hizo.

(3) Jumuiya ya Wabunge au Wawakilishi zitaweka kanuni zao za Uchaguzi wa watakaowawakilisha au watakaoingia katika nafasi mbali mbali zilizowekwa katika majimbo au mikoa au Kitaifa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba hii.

(4) Madiwani wote watajigawa kwa mpangilio ufuatao:-

(a) Diwani wa Kanda;

(c) Diwani wa Mikoa ambayo Kamati Kuu itaagiza kuwepo na kwamba kila kundi litachagua Mwenyekiti wake ambae atakuwa na dhamana na muwajibikaji Mkuu wa Madiwani wote wa kundi lake.

(5) Kiongozi wa Wabunge au wa Wawakilishi au wa Madiwani wanaotokana na Chama hiki watahakikisha kuwa Wabunge wote kutoka Chama hiki pamoja na Wabunge wa viti maalum, au wawakilishi wote kutoka Chama hiki pamoja na wawakilishi wa viti maalum au madiwani wote kutoka Chama hiki pamoja na madiwani wa viti maalum wanachangia chama kwa kila mwezi kutokana na mshahara wake pamoja na kuchangia katika malipo yake ya kiinua mgongo na posho za kumalizia muda (winding up allowance) kwa mujibu wa utaratibu utakaowekwa ndani ya Mkataba wao ambao utawekwa ndani ya Kanuni zitakazotungwa na Kamati Kuu na kuidhinishwa na Halmashauri Kuu.

## SURA YA TANO
## UCHAGUZI NA TARATIBU ZAKE
## KATIKA CHAMA, ELIMU KWA WANACHAMA

*Uchaguzi wa Viongozi wa Chama*

109. (1) Mgombea yeyote yule anaetaka kugombea nafasi yoyote ile ya Chama au ya Serikali kupitia tiketi ya Chama katika ngazi ya Tawi, Kata Jimbo, wilaya au Taifa atafuata utaratibu chini ya kanuni zitakazotungwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kwa ajili hiyo.

(2) Halmashauri Kuu ya Taifa inapoona inafaa itatunga Kanuni za Uchaguzi mara kwa mara kwa ajili ya chaguzi zilizoelezwa katika ibara ndogo ya (1) hapo juu au chaguzi nyingine zozote zinazoweza kutokea ndani ya Chama katika ngazi yoyote ile.

(3) Uchaguzi Mkuu wa Chama utafanyika kila baada ya miaka mitano, lakini chaguzi nyingine ndogo ndogo zinaweza kufanyika wakati wowote ule ambapo Halmashauri Kuu ya Taifa au Kamati Kuu ya Taifa itaelekeza.

(4) Pale ambapo Mkutano Mkuu umepelekwa mbele au kurudishwa nyuma kwa mujibu wa Ibara ya 70(1) na (2) na kwamba Mkutano huo umeambatana na uchaguzi wa ndani ya Chama basi viongozi wanaohusika wataendelea kushika nafasi zao hadi uchaguzi utapokamilika na shughuli zao zote zitakuwa halali kwa mujibu wa Katiba hii ila ijulikane pia kuwa endapo Mkutano Mkuu umerudishwa nyuma basi uchaguzi utafanywa hata kama kipindi cha miaka mitano hakijatimia.

*Wajibu wa Chama kuelimisha*

110. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa au Sheria nyingine yoyote ya nchi, Chama katika ngazi yoyote kitakuwa na wajibu na jukumu pale ambapo kimepata uwezo na nafasi ya kuwaelimisha wanachama wake kwa kadri itakavyowezekana mafunzo hayo yatalenga:-

a. Kujua, kujitambua na kuelewa elimu ya uraia na nidhamu ya kazi;
b. Kuheshimu na kukosoa mawazo ya wengine kwa misingi

ya ukweli na heshima kwa minajili ya kuweka nidhamu nzuri katika Chama;

c. Kuelewa haki yake ya kusikilizwa, kujitetea na kukata rufaa juu ya maamuzi yoyote yaliyochukuliwa dhidi yake;

d. Kutetea na kutekeleza usawa na haki mbele ya sheria kwa lengo la kuleta maelewano na utendaji wa kinidhamu katika Chama;

e. Kuelewa vyema haki na wajibu wa mwanachama kupiga kura na namna ya kulinda kura yake na ya viongozi wake na ya Chama chake wakati na baada ya kupiga kura;

f. Kuelewa kanuni zilizotungwa kuhusiana na uchaguzi wa Chama ndani ya chama na uchaguzi wa serikali na kuwa tayari wakati wowote kuziheshimu kanuni hizo na kuzifanyia kazi inapohitajika.

*Masharti ya kuchaguliwa na Kipindi cha Uongozi*

111. (1) Kipindi cha uongozi wa Chama kitakuwa miaka mitano kwa ngazi zote isipokuwa kama kiongozi huyo ameshindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa Katiba hii na Kanuni za Chama na iwapo kiongozi amechukua nafasi ya kiongozi aliyeondoka madarakani, kiongozi huyo atamalizia muda uliobaki kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kugombea kwa kipindi kingine.

(2) Iwapo kipindi cha uongozi kimemalizika na kuna sababu za msingi na za kitaifa kusababisha kwamba uchaguzi wa viongozi hao hauwezi kufanyika basi muda wa uongozi utaendelea kwa kipindi kingine cha miezi sita (06) na isiyozidi miezi kumi na mbili (12) na baada ya hapo ni lazima uchaguzi mpya uitishwe.

(3) Mwanachama wa Chama hiki atakuwa na fursa sawa na mwanachama mwingine yeyote ya kuchagua na au kuchaguliwa kushika nafasi ya uongozi katika Chama na Serikali kupitia Chama katika ngazi yoyote ile.

(4) Kiongozi anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) baada ya muda wake kumalizika, na hatoweza kuchaguliwa tena kwenye nafasi hiyo aliyofikia ukomo isipokuwa kama atagombea nafasi nyingine, isipokuwa tu masharti ya Ibara hii ndogo ya (4)

hayatatumika katika Uchaguzi wa nafasi za serikali kwa tiketi ya Chama ambazo hazijawekewa ukomo na Sheria husika.

(5) Mwanachama mpya wa Chama ataweza kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya uongozi katika Chama kwa ngazi yoyote ile, na pale ambapo pameanzishwa Tawi jipya na ambapo wanachama wa Tawi hilo wote ni wapya, basi viongozi wa muda wa Tawi watachaguliwa na watashika madaraka kwa kipindi kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi kumi na mbili (12) ambapo itabidi viongozi wa kudumu wa Tawi wachaguliwe.

## SURA YA SITA

## FEDHA ZA CHAMA, MAPATO NA MALI ZA CHAMA

*Fedha, Mapato na Mali za Chama*

112. (1) Chama kitajipatia mapato yake kutokana na vyanzo na njia zifuatavyo:-

a. Ada na viingilio vya wanachama;
b. Michango ya hiari ya wanachama na wafuasi wa Chama;
c. Ruzuku kutoka Serikalini;
d. Michango ya Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Madiwani na viongozi wengine wa Serikali wanaotokana na Chama kwa njia na utaratibu utakaowekwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa;
e. Misaada na ruzuku kutoka ndani na nje ya nchi;
f. Mikopo, ruzuku au misaada kutoka Chama, chombo, taasisi, mtu binafsi au mahali pengine popote ndani au nje ya nchi;
g. Mapato yanayotokana na hisa, miradi halali ya Chama, biashara, tafrija, michango au shughuli yoyote halali ama ya ndani au ya nje ya nchi;
h. Chanzo kingine chochote kile ambacho Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama itaidhinisha.

(2) Mali za Chama ni pamoja na:
a. Mali zote zinazohamishika na zisizohamishika;
b. Hisa za Chama katika miradi ya kiuchumi;
c. Mali za Ngome za Chama na Taasisi nyingine yoyote ilioanzishwa na Chama.

(3) Utaratibu wote ulioelezewa katika sura hii unaohusiana na fedha za Chama, mapato na mali za Chama utatekelezwa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Vyama Siasa pamoja na marekebisho ya sheria hiyo yatakayofanywa mara kwa mara na pia Chama kitatilia maanani Sheria nyingine za nchi zinazohusiana na masuala ya fedha, mapato na mali za taasisi.

(4) Bila ya kuathiri ibara nyingine yoyote ya Katiba hii kutakuwa na bajeti ya chama yenye kuonesha matumizi ya kawaida na ya kimaendeleo ya kila mwaka.

(5) Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Siasa kuhusu ruzuku ya serikali na matumizi yake na pia matumizi ya Chama kwa ujumla Katibu anaehusiana na fedha na uchumi wa Chama ataweka mahesabu yake vizuri kwa kila mwaka kwa ajili ya kukaguliwa na mkaguzi wa ndani na mkaguzi wa serikali, na baadaye ripoti ya ukaguzi huo kuwasilishwa kwa msajili wa vyama vya siasa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria zinazohusika.

*Malipo na Utaratibu wake*

113. (1) Malipo yote ya Chama ngazi ya Taifa yatawasilishwa katika ofisi ya Katibu Mkuu na kwa ngazi nyingine za Chama malipo hayo yatawasilishwa katika ofisi za Makatibu wa Chama wa ngazi husika.

(2) Halmashauri Kuu ya Chama inaweza kutunga Kanuni juu ya upatikanaji utoaji na utozwaji wa fedha kwa wanachama kwa njia ya mchango au vinginevyo pamoja na kubuni na kusimamia miradi ya uzalishaji ya Chama pamoja na kanuni za matumizi na udhibiti wa fedha na miradi hiyo.

(3) Kutakuwa na Kanuni za fedha za Chama zitakazotungwa na Halmashauri Kuu ya Chama Taifa zitakazoainisha utaratibu wa fedha ndani ya Chama kwa kuzingatia kwamba:-

(a). Kutakuwa na Idara ya Ukaguzi wa ndani wa Hesabu za Chama;
(b). Hesabu za Chama zitakaguliwa kila mwaka na Kampuni ya Wakaguzi wa Nje itakayoteuliwa na Kamati Kuu;
(c). Hesabu za Chama zitawasilishwa katika vikao vya Chama, Msajili wa Vyama vya Siasa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria;
(d). Katibu wa Fedha atatoa taarifa kwa umma kuhusu taarifa ya fedha ya Chama kila baada ya muda maalum kama itakavyoelekezwa na Halmashauri Kuu.

## SURA YA SABA

## MENGINEYO

## SEHEMU YA KWANZA

## MAREKEBISHO YA KATIBA NA KANUNI

*Marekebisho ya Katiba*

114. (1) Mkutano Mkuu wa Taifa unaweza, pindi ukiona inafaa kutunga, kurekebisha au kusahihisha Katiba ya Chama.

(2) Marekebisho ya Katiba ya Chama yatakuwa, kwa utaratibu na mpangilio ufuatao:

(a) Mapendekezo ya mabadiliko yoyote ya Katiba yatafanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa kabla ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.
(b) Mapendekezo yoyote ya mabadiliko ya Katiba yataanzia ngazi za ACT Tawi kwa wanachama kutoa maoni ambapo yataratibiwa na ngazi za Chama na

kisha kufikishwa katika ngazi za Kamati Maalum za Kamati Kuu kujadiliwa na kuchambuliwa na kuchakatwa kabla ya kufikishwa katika Kamati Kuu ya Taifa ambayo itayawasilisha katika Halmashauri Kuu itakayoandaa Rasimu ya mapendekezo kwa Mkutano Mkuu.

(c) Mkutano Mkuu ndio chombo pekee chenye mamlaka ya kubadili Katiba.

(3) Kwa madhumuni ya Ibara hii, marekebisho ya Katiba yanajumuisha:-
  (i) Kufuta na kutunga upya Katiba;
  (ii) Kurekebisha au kubadilisha sehemu ya Katiba au sura moja au sehemu ya sura hiyo; na
  (iii) Kuondoa neno, sentensi na badala yake kuweka upya neno au maneno, sentensi au sehemu ya sentesi katika Katiba hiyo.

(4) Pale ambapo pana makosa ya uchapaji au pamejitokeza upungufu wa herufi katika neno (printing or typographical error) na kwamba makosa hayo au upungufu huo umejitokeza baada ya Katiba hii kuchapwa basi makosa hayo na upungufu huo unaweza kusahihishwa wakati wowote ule baada ya kupata idhini ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(5) Maamuzi ya Ibara ya 114(1) ya Katiba hii yatakuwa halali iwapo thuluthi (2/3) ya wajumbe kutoka Tanzania Bara na thuluthi mbili (2/3) ya wajumbe kutoka Zanzibar waliohudhuria katika Mkutano Mkuu watayakubali na kuyaunga mkono marekebisho hayo.

(6) Katiba hii au marekebisho ya Katiba hii au sehemu ya Katiba hii inaweza kutafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza au kwa lugha nyingine yoyote panapo haja na ulazima wa kufanya hivyo lakini pale ambapo patatokea mgongano baina ya tafsiri ya Kiswahili na ile ya Kiingereza au lugha nyingine iliyotafsiriwa, tafsiri ya Kiswahili ndio itakayochukuliwa kuwa ni sahihi.

(7) Pale ambapo pana haja ya kuitafsiri Katiba hii yote kwa

lugha ya Kiingereza na kuifanya kuwa ni tafsiri halali ya Katiba, basi tafsiri hiyo itapaswa kwanza kuidhinishwa na Mkutano Mkuu Taifa.

*Kanuni za Chama*

115. (1) Bila ya kuathiri masharti ya vifungu vingine vya Katiba hii au masharti ya Sheria ya Vyama Vingi au Sheria nyingine za nchi, Kamati Kuu inaweza kutunga Kanuni za Chama au mwongozo wa Chama kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sera na malengo ya Chama kwa kuzingatia misingi ya Katiba hii.

(2) Kanuni zote zilizotungwa na Kamati Kuu zitapelekwa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya kuanza kutumika.

(3) Mgongano wowote utakaotokea baina ya Kanuni au mwongozo na Katiba au Sheria na Katiba ya nchi basi:-

(i) Katiba na Sheria za nchi zitachukua nafasi ya kwanza;
(ii) Katiba hii ya Chama itatamalaki mbele ya Kanuni na Miongozo ya Chama.

(4) Halmashauri Kuu inaweza ikiona kuna haja na ulazima wa kufanya hivyo kuzifanyia marekebisho au kuzifuta Kanuni au Miongozo hiyo ili kuendana na mahitaji ya wakati, na kwa madhumuni ya ibara ndogo hii, marekebisho ya Kanuni au Miongozo ni pamoja na;
(i) Kuzifuta zote na kuweka Kanuni au Miongozo mipya;
(ii) Kurekebisha au kusahihisha sehemu ya Kanuni au Miongozo hiyo na kuiwekea nyingine badala yake;

## SEHEMU YA PILI

## KUKAIMU MADARAKA, KUKASIMU MADARAKA, KUVUNJWA KWA CHAMA NA MAMBO MENGINEYO

*Kukaimu Madaraka*

116. (1) Pale ambapo mwanachama yeyote wa Chama mwenye madaraka kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, kwa sababu yoyote ile, hawezi kutekeleza kazi zake kwa

muda, au amesimamishwa au kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, mamlaka iliyo na uwezo wa uchaguzi au uteuzi wa nafasi hiyo inaweza kumteua mwanachama mwingine mwenye sifa zinazohitajika kukaimu madaraka hayo.

(2) Pale ambapo nafasi ya Katibu wa Mkoa iko wazi kwa sababu yeyote ile, Katibu wa Idara inayohusiana na Kampeni na Uchaguzi ndiye atakayekaimu nafasi ya Katibu wa Mkoa.

(3) Utaratibu wa kukaimu ulioelezwa katika Ibara ya 116(2) kwa Katibu wa Mkoa, utatumika pia kwa Katibu wa Jimbo, Kata, na Tawi.

(4) Kukaimu kwa madaraka hayo kutasita mara tu baada ya mtu aliyekaimiwa atakaporudi katika nafasi yake au mwanachama mwingine kuchaguliwa au kuteuliwa kujaza nafasi hiyo, na kwa vyovyote vile kukaimu huko hakutozidi vipindi viwili vya miezi sita kwa kila kipindi bila ya nafasi hiyo kujazwa kwa mujibu kwa masharti ya Katiba hii.

*Kuvunjwa Chama*

117. (1) kuvunjwa kwa Chama ni moja kati ya maamuzi muhimu na utaratibu wake wa upigaji kura utakuwa kama ulivyoelezwa chini ya ibara ya 75(4) na (5) ya Katiba hii.

(2) Katika tukio la kuvunjwa kwa Chama, Bodi ya Wadhamini wa Chama itahodhi mali zote za chama na kipaumbele kitakuwa ni kulipia madeni yote ya Chama. Endapo kutakuwa na salio lolote la mali ya Chama baada ya kulipa madeni yote, salio hilo litawasilishwa au kukabidhiwa kwa Taasisi yoyote ambayo shughuli zake zinalingana na misingi iliyoanzisha chama hiki kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Wadhamini.

(3) Katika tukio la kuvunjwa kwa Chama kwa nia ya kuungana na Chama kingine cha Siasa, Bodi ya Wadhamini wa

Chama itahodhi mali yote ya Chama na kuitumia mali hiyo kulipia madeni yote ya Chama. Endapo kutakuwa na salio lolote la mali ya Chama baada ya kulipa madeni ya Chama salio hilo litatumika kufuatana na azimio la kuvunja Chama ili kuungana na Chama kingine.

*Ofisi zilizoanzishwa*

118. Ofisi yoyote maalum itakayoanzishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa itasimamiwa na Afisa Mtendaji mwenye ujuzi wa kutosha kusimamia kazi za ofisi hiyo lakini italazimu Halmashauri Kuu ya Taifa ipeleke taarifa ya kuanzishwa kwa Ofisi hiyo katika kikao kinachofuata cha Mkutano Mkuu wa Taifa.

*Akidi na Uhalali wa Vikao*

119. (1) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Katiba hii:-

(a) Kiwango cha wajumbe cha kuhalalisha kikao chochote cha Chama katika ngazi yoyote ile itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa kikao hicho.

(b) Vikao vyote vitaendeshwa na Mwenyekiti wa kikao husika na ikiwa hayupo kikao kitaendeshwa na Makamu wa Mwenyekiti, na yeye ikiwa hayupo basi wajumbe wa Kikao hicho watamchagua, kwa wingi wa kura mjumbe mwingine yeyote ili awe mwenyekiti wa muda.

(c) Wajumbe wanaweza kuitisha kikao chochote endapo tu asilimia sabini na tano ya wajumbe wa kikao hicho watatia saini kuhitaji kikao hicho kiitishwe;

(d) Bila kuathiri yaliyomo katika ibara ndogo ya (9) hapo juu, wajumbe wanaohitaji kikao hicho lazima waoneshe kuwa viongozi katika ngazi husika wameshindwa kuitisha vikao hivyo zaidi ya mara tatu kwa mujibu wa Katiba nao utaratibu wa kuitisha vikao vya namna hiyo utafafanuliwa kwenye Kanuni za Chama.

(5) Uamuzi wowote ule utafikiwa kwa zaidi ya nusu ya kura za wajumbe halali wa kikao husika.

(6) Ibara ndogo ya (2) ya ibara hii haitoathiri uamuzi unaofikiwa kwa njia ya muafaka au maridhiano.

(7) Katika shughuli za uchaguzi wowote ule kura zitakuwa za siri.

(8) Masharti ya kifungu hiki hayotoathiri masharti ya vifungu vingine vyovyote vya Katiba hii ambavyo vimetoa masharti ya upigaji kura juu ya suala lolote.

*Mialiko kwa wadau, Wataalam na watu wengine*

120. Kikao chochote cha Chama katika ngazi yoyote ile kitakuwa na uwezo wa kuwakaribisha watu wasiokuwa wajumbe wa kikao hicho, ikiwa ni pamoja na wataalamu na wadau, kwa madhumuni ya kuwasikiliza au kwa ajili ya kupata ushauri wa kitaalamu au ushauri mwingine kutoka kwao ambapo watu au wadau waliokaribishwa hawatakuwa na haki ya kushiriki katika kutoa maamuzi au kupiga kura.

*Uwezo wa Kuunda Kamati*

121. (1) Kikao chochote cha Chama katika ngazi yoyote ile kinaweza, kuunda Kamati na/au Tume ya muda kwa ajili ya kuchunguza jambo au kufanya shughuli yoyote itakayoelekezwa kufanywa na kikao chenyewe kwa kuzingatia kwamba Tume iliyoundwa ni lazima kupewa majukumu yaliyo wazi (hadidu za rejea) na kupewa muda wa kukamilisha kazi yake.

(2) Uhalali wa Kamati na/au Tume ya muda utakwisha pale inapowasilisha taarifa yake na kupokelewa na kikao kilichoiunda, isipokuwa muda wa Kamati au Tume ya muda unaweza kuongezwa na kikao kilichounda ikiwa pana haja hiyo.

*Wajibu wa Kiongozi wa Serikali kwa tiketi ya Chama*

122. (1) Kiongozi yeyote wa serikali kwa tiketi ya Chama atawajibika kusaini mkataba wa ahadi kwa Chama na atalazimika kufanya mambo yafuatayo: -

a. Kukichangia Chama kwa utaratibu utakaowekwa kwa mujibu wa Kanuni zilizotungwa na Kamati Kuu na kuthibitishwa na Halmashauri Kuu;
b. Kushiriki katika shughuli zote za Chama;
c. Kutunza maadili na taratibu za Chama;
d. Kutoa taarifa za utendaji wa shughuli zake za kikazi mbele ya Kamati Kuu au Sekretarieti ya ngazi yake inayomhusu; na
e. Kufanya jambo jingine lolote atakaloagizwa na Chama, kwa utaratibu maalum utakaowekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(2) Ikiwa kiongozi hatatekeleza moja au zaidi ya moja ya mambo yaliyoainishwa katika ibara ndogo ya (1) hapo juu, Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kumchukulia hatua yoyote ya kinidhamu kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama zinazohusika.

*Mahudhurio ya Kikao cha Chama*

123. (1) Mjumbe wa kikao anawajibika kuhudhuria mikutano yote ambayo yeye ni mjumbe na pale ambapo hatohudhuria kwa sababu maalumu itambidi amuarifu katibu wa kikao hicho kwa njia za mawasiliano zinazokubalika pamoja na sababu za kutokuhudhuria kwake.

(2) Mjumbe anayekosa kuhudhuria vikao vitatu (3) mfululizo ambavyo anatakiwa kikatiba ahudhurie bila ya sababu inayokubalika basi atasita kuwa mjumbe wa kikao hicho hadi hapo atakapojadiliwa na kikao kinachohusika na ama kusamehewa au kuchukuliwa hatua za kinidhamu kama zilivyoelezwa chini ya kifungu cha 103 (3)(i)(iii) na (iv).

*Kujaza nafasi zilizowazi*

124. Pale ambapo pana nafasi wazi ya mjumbe katika kikao chochote na cha ngazi yoyote ya Chama, mamlaka inayohusika itajaza nafasi hiyo kwa haraka, na kwa vyovyote si zaidi ya miezi sita (6) kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

*Ofisi za Viongozi wa Chama*

125. (1) Kiongozi wa Chama, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Chama, Mshauri Mkuu wa Chama, Makatibu na Manaibu Makatibu wote wa Kamati za Chama watakuwa na ofisi zao katika Makao Makuu ya Chama, na/au Ofisi Kuu ya Chama, lakini kiongozi yeyote aliyetajwa katika ibara hii anaweza kufungua ofisi ya muda au ya kudumu katika sehemu nyingine ya nchi pindi akipata idhini ya Kamati Kuu ya Taifa.

(2) Waratibu wa Kanda watakuwa na ofisi zao katika eneo lolote lililomo ndani ya kanda hiyo.

*Upeperushaji wa Bendera ya Chama*

126. (1) Makao Makuu ya Chama, Ofisi ndogo ya Chama, Ofisi za Kanda za Chama, Matawi ya Chama, Ofisi za Ngome za Chama pamoja na maeneo mengine yoyote ambayo shughuli za Chama zinafanyika zitaperusha bendera ya Chama juu ya Mlingoti.

(2) Viongozi wafuatao wa Chama watapeperusha bendera ya Chama katika magari yao, na ikiwa wakipenda kwenye majumba yao;

(i) Kiongozi wa Chama;
(ii) Mwenyekiti wa Chama;
(iii) Makamu Mwenyekiti;
(iv) Katibu Mkuu;
(v) Naibu Katibu Mkuu;

*Kukasimu Madaraka*

127. (1) Madaraka, uwezo na nguvu za Chama zinaweza kukasimiwa kutoka kikao cha juu kwenda kikao cha chini

(2) Mkutano Mkuu wa Taifa unaweza kukasimu madaraka yake kwa Halmashauri Kuu ya Taifa isipokuwa tu yale majukumu ambayo hayawezi kukasimiwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria nyengine za Nchi

(3) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati Kuu ya Taifa isipokuwa kwa mashariti yale yale yalioelezwa chini ya Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii

*Uteuzi na masuala ya Kijinsia na makundi maalum*

128. (1) Pale ambapo chombo cha chama kimepewa au Kiongozi yeyote wa chama amepewa mamlaka ya uteuzi katika nafasi yoyote ile, basi:-

(a). Ikiwa nafasi ya kijinsia au utaratibu wa kijinsia haukuwekwa katika ibara inayohusika na uteuzi huo, basi ni lazima kwa chombo hicho au kwa mteuzi huyo kuzingatia jinsia ambayo anahisi inafaa lakini kwa vyovyote vile isipungue asilimia ishirini na tano (25%) ya idadi ya wateuliwa wote katika nafasi au sehemu hiyo.

(b). Katika utaratibu huo huo wa uteuzi, chombo hicho au kiongozi huyo mwenye mamlaka ya uteuzi atazingatia pia umuhimu wa kuwepo kwa nafasi ya mlemavu angalau katika baadhi ya vyombo vya chama.

(2) Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kutunga Kanuni juu ya utekelezaji bora wa ibara hii kuhusiana na suala la jinsia na makundi maalum.

## SEHEMU YA TATU

## TAFSIRI YA MANENO MBALI MBALI NA UFAFANUZI WA BAADHI YA MANENO

*Ufafanuzi na tafsiri ya maneno mbalimbali*

129. Katika Katiba hii, maneno yafuatayo yatakuwa na maana iliyopewa mbele yake isipokuwa pale ambapo imeelezwa vyenginevyo.

(a) “Chama” Maana yake ni “ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY na kwa kifupi “ACT” au '’ACT-Wazalendo”

(b) “Haki za Binaadamu” ni haki ambazo mtu yeyote anakuwa nazo tangu kuzaliwa kwake, na ni kama zilivyotangazwa katika Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu.

(c) “Haki za Watu” ni haki za watu ambazo hutangazwa mara kwa mara na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, au Jumuiya nyinginezo zinazotambulika duniani.

(d) “Katibu Mkuu” ni Katibu Mkuu wa Chama ambaye ndiye mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Chama Kitaifa.

(e) “Kijana” inajumuisha kijana yeyote bila kujali jinsia ambaye atakubalika na Chama kuwa ni kijana, na kama itakavyoelezwa katika Kanuni za Ngome ya Vijana.

(f) “Kukaimu madaraka” ina maana ya kumshikia kiongozi nafasi yake ya kazi mpaka hapo mwenye nafasi hiyo ataporejea kazini au hadi hapo nafasi hiyo itakapojazwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(g) “Idara ya Chama” ina maana ya Idara ya Chama katika ngazi ya mbali mbali na inajumuisha Idara za Ngome.

(h) “Makamu Mwenyekiti” ina maana ya Msaidizi na Mshauri wa Mwenyekiti Taifa.

(i) "Mwenyekiti wa Taifa" ina maana ya msimamizi Mkuu wa Chama Kitaifa.

(j) "Mkutano Mkuu" ina maana ya mamlaka ya juu kabisa ya Chama yenye maamuzi ya mwisho katika ngazi inayohusika ya Chama.

(k) ''Kiongozi wa Chama" ina maana ya Mkuu wa Chama ambaye ana jukumu la kudhibiti sera za Chama pamoja na kutoa miongozo inayohusiana na sera.

(l) "Liwali wa Chama" ina maana ya kiungo cha Chama baina ya uongozi wa Tawi na wananchi wa eneo lenye mkusanyiko wa wananchi.

(m) "Mratibu wa Chama" ina maana ya kiungo cha Chama baina ya eneo la Kanda aliyopo Mtaribu huyo na ngazi ya Taifa.

(n) "Mtumishi wa Chama" ina maana ya mwanachama aliyeteuliwa au kuchaguliwa kushika wadhifa wa uongozi au utendaji katika Chama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(o) "Mzee" ina maana ya mwanachama wa Chama aliyefikia umri wa miaka khamsini (50) au zaidi kwa mwanamke, au miaka khamsini na mitano (55) au zaidi kwa mwanamme.

(p) "Miongozo" ina maana ya maelekezo yanayowekwa Utaratibu wa namna ya utekelezaji wa jambo fulani inayowekwa na Kamati Kuu

(q) "Viongozi Wakuu wa Kitaifa" ina maana ya Kiongozi wa Chama, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Chama

(r) "Viongozi wa Kitaifa" ina maana ya Manaibu Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Chama, Mshauri Mkuu wa Chama Wajumbe wa Kamati Kuu, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Makatibu na Manaibu Makatibu wa Chama katika ngazi ya Taifa, wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama, Mwenyekiti na Katibu wa Ngome za Chama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili

(s) "Kiongozi wa Serikali" ni pamoja na:-

    (i) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano atokanaye na Chama.

(ii) Rais wa Zanzibar na Makamu wa Rais wa Zanzibar atokanaye na Chama.
(iii) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano atokanaye na Chama
(iv) Waziri atokanaye na Chama
(v) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atokanaye na Chama
(vi) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar atokanaye na Chama
(vii) Spika au Naibu spika wa Bunge na Spika au Naibu spika wa Baraza la Wawakilishi atokanaye na Chama
(viii) Diwani na Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya au Mji atokanaye na Chama
(ix) Kiongozi wa serikali ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa atokanaye na Chama
(x) Meya au Naibu Meya atokanae na Chama.

(t) "Kutunga" ni pamoja na kufuta, kurekebisha, kubadilisha Katiba hii, ama kuongeza au kupunguza sehemu ya Ibara yaKatiba hii pamoja na kutunga Kanuni, kuzifanyia marekebisho, kuzifuta na kuweka Kanuni mpya.
(u) Kila inapotajwa moja itafsiriwe kama ni wingi na kila penye wingi itafsiriwe vile vile kama ni moja.
(v) Kila penye neno la jinsia ya jinsia ya "kike" lisomwe pamoja na neno la jinsia ya "kiume" na hivyo hivyo kila penye neno la jinsia ya "kiume" pasomeke na neno la jinsia ya "kike".
(w) Kila anapotajwa mtu mwenye dhamana ya kazi fulani kwa kutaja madaraka ya kazi yake ifahamike kuwa mtu anayehusika ni pamoja na mtu yeyote yule anayekaimu au aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kushikilia dhamana ya kazi hiyo.
(x) "Ngome" ni kitengo cha Chama cha Wanawake, Vijana au Wazee
(y) Kila penye neno "ibara" basi isomeke kuwa ni "kifungu" na kinyume chake; na maneno "ibara ndogo" kifungu kidogo yatatafsiriwa kwa ulingano huo huo.

(z) "Sekretarieti" ina maana ya "Kamati Tendaji" ya chombo kinacho husika

## SEHEMU YA NNE

## JINA LA KATIBA TAREHE YA KUTUMIKA NA UHALALISHAJI WA MAMBO YALIYOKWISHA KUFANYWA CHINI YA KATIBA HII KABLA YA KUFANYIWA MAREKEBISHO

*Jina la Katiba na kuanza kutumika*

130. Jina la Katiba hii ni **Katiba ya Alliance for Change and Tranpsarency (ACT- WAZALENDO) ya mwaka 2015 toleo la 2020** na kwa kiingereza ni "The Constitution of the "Alliance for Change and Transparency, 2015 – (2020 Edition)", itaendelea kutumika pamoja na marekebisho yake mara tu baada ya Mkutano Mkuu kuyapitisha.

*Utekelezaji wa Ibara mbali mbali*

131. Utekelezaji wa masharti ya ibara mbalimbali za Katiba hii zinazohusu marekebisho ya uchaguzi na, au uteuzi wa wajumbe wa vikao vya Chama katika ngazi mbali mbali hautaathiri uchaguzi na, au uteuzi ambao umekwishafanyika katika uchaguzi wa Chama ndani ya Chama uliokwisha malizika wakati marekebisho haya yanapitishwa.

*Kuhalalisha mambo fulani*

132. Jambo lolote lililofanywa au kutokufanywa kabla ya marekebisho ya Katiba hii, litaendelea kuwa halali chini ya Katiba hii mpaka pale ambapo jambo hilo au kitendo hicho kitakapokuwa kimerekebishwa au kubadilishwa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba hii, na kwamba uteuzi uchaguzi, uamuzi au maelekezo mengine yoyote yaliyofanywa kabla ya marekebisho haya ya Katiba bado yatakuwa ni halali na yenye nguvu za kikatiba hadi pale uteuzi au uchaguzi mwingine au uamuzi mwingine au maelekezo mengine yoyote yatakapokuwa yamefanywa au yametolewa chini ya matakwa ya marekebisho ya Katiba hii.

*Uhalalishwaji wa kanuni*

133. Kanuni zozote zilizotungwa chini ya Katiba hii kabla ya marekebisho zitaendelea kutumika, na zitakuwa halali na zenye nguvu kamili kama kwamba zimetungwa chini ya Katiba hii mpaka pale kanuni hizo zitaporekebishwa au kubadilishwa kwa mujibu wa matakwa ya marekebisho ya Katiba hii.

*Usawazishaji wa makosa ya uandishi au uhamisho wa Ibara kabla ya kuchapwa Katiba*

134.(1) Pale ambapo Katiba hii inataka kuchapwa, Mwanasheria Mkuu wa Chama atakuwa na uwezo ambao hauwezi kukasimiwa kwa mtu yeyote yule wa:-

(a) Kufanya masahihisho yote yaliyojitokeza yanayohusika na makosa ya uandishi;

(b) Kufanya masahihisho ya Ibara au ibara ndogo za Katiba hii kwa kuzipanga vizuri, au kwa kuzichanganya kuwa moja au kwa kuzitohoa kuwa mbalimbali;

(c) Kufanya uhamisho wa baadhi ya Ibara au Ibara ndogo kwa kadri itakavyokuwa ama kwa kuzipeleka mbele au nyuma na kuzipa namba nyingine za Ibara hizo au Ibara ndogo hizo;

(d) Kufanya jambo jingine lolote lile ambalo ni kwa ajili ya kuiweka vizuri Katiba hiyo ili iwe na mtiririko mzuri wa kusomeka na wenye kueleweka.

(2) Pale ambapo masahihisho hayo au uhamisho huo wa Ibara au Ibara ndogo chini ya Ibara ya 134(1) (a), (b), (c) na (d), Mwanasheria Mkuu wa Chama atahakikisha kuwa, hayabadilishi maana yeyote ile ya Ibara hiyo au hayaleti tofauti yoyote ile ya maana katika Ibara yoyote ile ya Katiba hii.

(3) Kama kuna maamuzi yoyote yale yaliyofanywa au hatua yoyote iliyochukuliwa kwa kutumia Ibara ambayo imebadilika kuwa ya nyuma au mbele zaidi baada ya masahihisho hayo, basi maamuzi hayo yaliyofanywa au hatua hiyo iliyochukuliwa na kuzifanya Ibara hizo kusomeka tofauti baada ya kuchapwa Katiba hii, yatakuwa halali na yatatafsiriwa kama yamefanywa chini ya Ibara hiyo iliosahihishwa au iliyopelekwa mbele au nyuma.